Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele

Asante, ndugu. [Ndugu Samuel Johnson anasema, "Mungu akubariki, Ndugu Branham."—Mh.] Jamani, ingenibidi kuishi, kuishi maisha yenye sifa namna hiyo, sivyo? Hakika ninathamini hilo, hata hivyo. Kama hakukuwa na mtu aliyeamini, ingenifaidi nini kuenda? Naam. Huna budi kuwa na mtu wa kuamini. Haijalishi kile Mungu angeweza kufanya, ikiwa huamini kile anachofanya, basi. . .Haina budi kuwa ni sisi wawili, unajua, mtu fulani hana budi kuamini pamoja nami kwa ajili ya hili. Pia haijalishi ni nini kingetukia, ikiwa—ikiwa hakuna mtu anayeamini, basi isingekuwa na faida yoyote, isingekuwa na maana hata kidogo. Bali nina furaha sana kusikia kwamba watu wangali wanaamini hadithi hii ya kupendeza ya Bwana Yesu. Yeye ni upendo mzuri kwetu sote.

2 Nami nilikuwa na wakati mzuri sana jana usiku. Ni—nilienda nyumbani na kuishi kwa matokeo yake hadi wakati huu. Nimerudi kujaza tena. Nami ninafikiri hiyo ndiyo sababu yetu sote kuja, ni kusikia nyimbo za Sayuni, shuhuda za watu, na katika nyumba ya Bwana.

3 Sasa, ninaamini ilisemwa wakati mmoja, katika Biblia, "Jinsi ilivyo vema kwamba ndugu wakae pamoja kwa umoja." Ni kama mafuta ya kutia yaliyokuwa kwenye ndevu za Haruni, yaliyoshuka mpaka upindo wa vazi lake. Nafikiri hakuna kitu chenye thamani zaidi ya kuona wa—watu walio na umoja, katika Roho wa Bwana, kuwa umoja, wote wakikubaliana.

4 Mnajua, nafikiri zile siku kumi walizokuwa wakingojea i—ile ya asili, kumwagwa kwa kwanza kwa Roho Mtakatifu, jinsi huo hapana budi ulikuwa ni wakati wa kuunganisha, kwa watu hao wote katika nia moja na mapatano. Na kila wakati ambapo watu wanaungana namna hiyo, tangu wakati huo, Roho Mtakatifu daima hukutana nao.

5 Biblia ilisema, Yesu akinena, alisema kwamba, "Popote wawili ama watatu wamekusanyika katika Jina Langu, hapo nipo katikati yao." Kwa hiyo sasa tunajua, kwa kweli, kwamba Yesu amekutanika pamoja nasi, kwa sababu tumekusanyika katika Jina Lake.

6 Sasa, usiku wa leo, umetolewa kwa ajili ya kuwaombea watu wagonjwa. Na wakati nilipokuwa ninakuja kuingia mlangoni, niliona kulikuwa na wale waliolala hapo, ambao walikuwa wagonjwa na wanateseka. Mwanangu ndiyo kwanza arudi kutuchukua mimi na Dada Moore, na kutuleta huku kanisani;

na alisema alikuwa amesambaza kadi za maombi, kwa hiyo aliweza kuzipa namba na—na kuwaleta watu mmoja mmoja, kuwaombea.

7 Leo nilikuwa na siku nzuri sana. Nilikuwa huko chini katika bu—bustani ndogo hapa chini, na kulikuwa na mtu aliyekuwa anakuja, akikusanya ta—takataka kutoka kwenye pipa la takataka.

Nikasema, “Nipo hapa kwa ajili ya mkutano.”

Akasema, “Loo, hapo juu kwenye uwanja wa kambi?”

Nikasema, “Naam.”

8 Akasema, “Vema,” akasema, “Ninaenda huko juu kesho usiku.” Akasema, “Yupo mhudumu, Ndugu Branham, anaenda kuhubiri.”

Nami nikasema, “Naam, bwana.”

9 Naye akasema, “Vema,” akasema, “Ninataka kwenda huko juu.” Kasema, “Mke wangu na familia walikuwa huko juu jana jioni.” Na—na m—mtu huyo alikuwa akivuta sigara.

10 Ndipo—ndipo nikasema, “Vema,” nikasema, “je! unamjua Ndugu Branham?”

11 Kasema, “Loo, imekuwa ni miaka mingi iliyopita.” Kasema, “Alikuwa hapa kwa ajili ya . . . daima nimewazia kwamba ilihitaji ujasiri mwingi, au imani, au kitu fulani.” Kasema, “Nilikuwa huku kwenye ghala la silaha kumwona akiwaleta wale watu huko juu, kwenye vitanda vya wagonjwa na machela, na vipofu na waliopindika, na kuwaona wakitembea kutoka jukwaani.”

Lakini mimi—mimi nikasema, “Mimi—mimi ni Ndugu Branham.”

12 Ndipo a—akasema, “Loo, mimi si . . . ” Kwa namna fulani akaweka sigara yake nyuma. Na namna ya mtu mwungwana sana. Ndipo mtu mwingine akatokea, mwema sana.

13 Tulikuwa na mazungumzo mafupi, nilikuwa nikiwaelezea kuhusu Uwepo wa Mungu. “Ha—hakuna ma—mahali uwezapo kutazama. Unaweza kutazama mti, unaweza kuona unadhibitiwa na Mungu. Na kila kitu unachoona ni Mungu.” Nikasema, “Ninatumaini tukikutana tena, maishani, kwamba utakuwa Mkristo kama familia yako.” Nikawaombea punde tu walipoondoka, yule mwungwana mwingine.

14 Na kama wapo hapa usiku wa leo, natumai siwaaibishi kwa kusema hili, bali ni—ni—ninatumaini kwamba Mungu atawafanya watu hao wawili wote kuwa Wakristo. Tunataka kukutana tena katika nchi iliyo bora, ambapo Mti wa Uzima unanawiri ng’ambo ile ya mto. Sisi sote tunajua tunakuja njia hiyo.

15 Na sasa nikipitia tu masoko na mahali, na kurudisha kumbukumbu za kale. Basi jana jioni wakati nilipokuwa nikiondoka, Ndugu Johnson alikuwa ameketi pale nje, ndugu, yeye na Dada Johnson. Sijawaona kwa miaka mingi. Mara ya mwisho nilipomwona, alipatwa na kiharusi, alikuwa amepooza. Ilikuwa ni huko California, Ndugu Noel. Inaleta kumbukumbu za siku zilizopita, kuja kwa kwanza Arkansas, mji mdogo unaoitwa Moark, kanisa dogo la Kipentekoste lililokalia upande mmoja. Moja kwa moja kuteremka kwa Ndugu . . . huko Corning, Arkansas, Ndugu Johnson na mke wake. Na jinsi ninavyokumbuka siku hizo adhimu!

16 Kisha moja kwa moja chini kwa Ndugu T. Richard Reed. Ninakumbuka asubuhi hiyo, huko chini Jonesboro, mke wake, alikuwa ni tasa. Alitaka watoto.

17 Nilikuwa huko nyuma kwenye chumba, na watu walikuwa wamerarua pazia kutoka dirishani, wakiingia, nikiwaombea wagonjwa. Aliniweka huko nyuma katika chumba. Ningefanyiza mstari wa maombi. Alidhania niliingia ndani na kwenda kulala, na kungekuwa na watu wakisimama huku na huko kwenye uga wa nyuma, kuwa na mstari wa maombi. Na yeye akiwa huko nje amelala; nilikuwa huko nyuma nikiombea wagonjwa, kupitia dirishani.

18 Nami ninakumbuka, asubuhi iliyofuata, nikitoka. Na Dada Reed alikuwa amepata matibabu na kila kitu, kujaribu kuwa na mtoto. Ndipo nikaanza kutembea kupitia kwenye milango, mojawapo ya maono ya kwanza katika mkutano, nilimwona amemshika maskini mtoto mvulana mwenye nywele nyeupe. Nilinena katika Jina la Bwana kwamba atampata. Alimpata, na jinsi Mungu alivyoibariki nyumba yao.

19 Na, loo, mambo mengi sana! Na Ndugu G. H. Brown; Little Rock hapa chini. Ninakumbuka huko, Mtaa wa Victor wa 505.

20 Mnajua, ni—ningependa tu kuchukua mfululizo wa mikutano na kujiandama mwenyewe kurudi kupitia kote, katika Arkansas na hayo makanisa na kadhalika, na kuwaona watu, na kupeana mikono nao. Hilo ni jema sana, watu wa Mungu! Kila mahali ambapo nimeenda, nimekuwa huko chini katika misitu ya Afrika, na huko miongoni mwa Wahindi, wala-moto, na wachawi, na kote kupitia mataifa, na kuzunguka ulimwengu, bali sijawahi kuwasahau rafiki zangu walioko Arkansas, jinsi ambavyo wangeshika mikono hiyo, na kuwalaza watoto wao chini ya lori wakati ilikuwa ikicheza . . . ikinyesha. Kuona wasichana wadogo wakitembea kuteremka mtaani, mguu tupu, ama kuteremka barabarani, na halafu wanapangusa vumbi kutoka kwenye miguu yao na kuvaa viatu vyao na soksi ndefu, wanaingia ndani. Mimi huko nyuma vichakani, nikiuombea mkutano. Kamwe sitasahau hayo, kile watu halisi wa kweli

walicho. Mimi. . .ninayo tu shukrani sana kwamba kungali na watu kama hao ulimwenguni.

21 Usiku wa leo, nilikuwa nimesahau kuhusu kunibidi kuja kwenye mkutano huu hivi majuzi, na imevuta tu, imevuta kwa nguvu. Hivi majuzi ninii. . .mmoja wa mameneja wa mkutano ambaye hushughulikia barua za kigeni, aliingia na—na mialiko mia sita za nchi za kigeni, na haja nyingi; kando na, kitabu kinene *hivi*, katika miezi sita iliyopita, kimekuja kwa ajili ya sehemu mbalimbali. Laiti ningaliweza kwenda kwa kila moja ya hizo. Bali kwa kawaida mimi hujaribu tu kuenda jinsi Bwana anavyoniongoza. Sijawahi kuacha mikutano yangu iwe mikubwa. Mimi ningali maskini yule jamaa wa kale aliyekuja wakati mmoja. Hainibidi kuwa na pesa zozote. Sina mipangilio yoyote mikubwa ya kudhamini. Sihitaji pesa zozote hata kidogo. Bwana hushughulikia hayo, kama alivyofanya mwanzoni.

22 Tofauti ya pekee usiku wa leo, nilikuwa tangu wakati nilipokuja Corning, ninaamini nilikuwa na m—mfuko ulioraruka, ambao kaka yangu alikuwa amenipa suti aliyokuwa nayo. Jamaa mdogo, na a—aliurarua. Na—nami. . .Ulikuwa kwenye upande wa mkono wa kuume, na kurarua mahali pakubwa nyuma. Mimi na mke wangu tulienda chini kwenye duka la malimali na kununua baadhi ya viraka hivi unavyoshikilia kwa pasi, mwajua, bali isingepiga pasi kwenye mfuko huu. Kilizidi kutoka. Ndipo nikachukua uzi na kupashona. Haikuwa kazi nzuri sana. Sikuwa na koti wakati huo, na ninakumbuka ilikuwa inabidi kushikilia mkono wangu wa kulia juu ya mahali hapo paliporaruka, na kusalimiana kwa mikono na rafiki zangu wahudumu kwa kutumia mkono wangu wa kushoto, kuzuia kuonekana kwa hilo koti. Ndipo nikasema, "Samahani mkono wa kushoto, uko karibu zaidi na moyo wangu." Vema, ninalo koti bora usiku wa leo, lakini ningali ninawatakeni karibu na moyo wangu. Mmekuwepo muda wote. Ninampenda Bwana Yesu kama tu nilivyompenda wakati huo.

23 Na nimekuwa na majaliwa ya kuzungumzia watu laki tano kwa wakati mmoja. Nimeona miito ya madhabahuni, kadiri ya wenyeji elfu thelathini wanaovalia blanketi wakitoa mioyo yao kwa Yesu Kristo kwa wakati mmoja, wakapasua sanamu zao sakafuni. Nimeona miujiza elfu ishirini na tano ya kipekee ikifanyika katika kipindi cha sekunde moja, kwa ombi moja, huko Durban, Afrika Kusini; ambapo malori kumi na sita yaliyojaa viti vya magurudumu, vitanda vya wagonjwa na machela—machela yaliteremka mtaani.

24 Siku iliyofuata, wakati Sidney Smith, meya, aliponiambia niende; aliniita huko, kasema, "Nenda kwenye chumba na utazame nje kuelekea Bahari Hindi huko." Na hapo wakashuka, wenyeji waliokuwa wakipigana vita wenyewe kwa wenyewe; wamelazwa kwenye vitanda vya wagonjwa na machela, vitu vilivyotengenezwa nyumbani walivyokuwa wamewaleta

kwavyo, siku iliyotangulia; na hapa walikuwa wakiteremka nyuma ya haya malori kumi na sita yaliyojaa, wakiimba, "Amini tu! Mambo yote yanawezekana, amini tu."

25 Inakufanya uwazie, "Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika kuwa tamu, iliyomwokoa mwovu kama mimi." Kujua kwamba nina ushirika na watu kama hao, kuishi hapa duniani na katika Umilele, pamoja.

26 Nayahesabu haya kuwa ni majaliwa makubwa, katika kampeni yenu, ama hapa katika mkutano wenu. Nimeheshimika pakubwa kuzungumza kwenye moja ya mikutano yenu hapo kesho, kwenye adhuhuri nafikiri ndivyo, na kuanzia saa sita hadi saa sita u nusu, ama kitu kama hicho, kesho. Bwana akipenda, ninataka kuwa hapa nikiwa tu na Ujumbe mdogo rahisi wa Injili.

27 Usiku wa leo sasa, kuombea wagonjwa. Sininii. . .Upako wa kuwaombea wagonjwa ni. . .Ni Roho yule yule, ila upako tofauti unapowaombea wagonjwa, mbali na ulivyo kwa njia hii. Sijakula tangu mapema leo. Basi nimekuja kwenye jengo, nikifunga, nikiomba. Na—na sitaki kuwa nikihubiri ili nipate kuwa chini ya upako kama vile wakati ndugu zangu wahudumu, kuhubiri. Na—nataka kuhisi Uwepo wa Bwana ninapowaombea wagonjwa, maana kila mmoja nitakayemwombea, usiku wa leo, ni—ninataka iwe, ninataka waponywe. Ni—ninataka hilo kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwamba—kwamba Mungu atawaponya wagonjwa. Nami ninaamini Yeye atafanya hivyo.

28 Kwa hiyo ili kufanya hili, na wengi wenu labda hamjawahi kuwa kwenye mkutano hapo kabla, na wengi wenu hawajaizoea huduma. Baadhi yenu mnakumbuka wakati nilipokuwa hapa mara ya kwanza katika Arkansas. Ilibashiriwa, mnakumbuka. Ninawashika watu mikono, nami ningeshika tu mikono yao hapo kwa dakika chache, ndipo basi Bwana angenena na angesema hasa kile walichokuwa nacho. Ndipo nikawaambia kwamba Yeye aliniambia, wakati alipokutana na mimi, kwamba, "Wewe, kama utakuwa mwaminifu, kwamba itapanda juu tena na utajua siri yenyewe ya mioyo yao." Ni wangapi waliopata kunisikia nikisema hilo kabla halijatukia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, ilienda kwenye hilo. Sasa imeenda zaidi. Inazidi tu. . .Bwana anazidi kubariki, na sisi tunashukuru tu kwa hilo.

29 Kwa namna fulani, mimi si mhubiri; yeyote anajua hilo. Mimi, mimi ni—mimi ni tairi ya akiba. Unatumia tairi ya akiba wakati umepata. . .Hatuna tairi zilizotoka pumzi, hata hivyo. Sasa sisi, imetokea tu kwamba ninakuja, nao wanataka tu kubingirisha tairi ya akiba kwa muda kidogo. Lakini mimi—mimi ni mhudumu tairi ya akiba, kwa sababu sina elimu ya kuwa mhubiri; sikuenda shule yoyote ya Biblia. Lakini kile nijuacho kumhusu Yesu Kristo, ninapenda kukieleza katika

njia yangu mwenyewe dhaifu, na Mungu ameiheshimu. Pia ninatumaini, usiku wa leo, kwamba katika njia ile ambayo Yeye alinituma kuwahudumia watu, hiyo ni kuwaombea wagonjwa, kwamba Yeye atajithibitisha Mwenyewe mbele zenu usiku wa leo, kwamba Mungu yule ninayempenda na nyinyi mnampenda yu pamoja nasi usiku wa leo.

30 Hebu sisi sasa kwa ajili ya Ujumbe mdogo wa kawaida. Usipoleta Ujumbe mbele za watu, mtu fulani haelewi. Wataondoka na kusema, "Sijawahi kusikia kama huo. Ninajua hakuna kitu kama hicho katika Biblia."

31 Kwa hiyo ili ku—kulikaza hili, ni—ninawatakeni msikilize kwa makini sana sasa, kwa dakika chache, wa anwani ya Ujumbe mdogo wa kawaida, mada ya kampeni: *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*. Sasa kumbukeni anwani hiyo, kwamba: *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*.

32 Na mimi ningependa kuuliza hili, kabla sijasoma, je! mnaweza kunisikia vizuri? Mtu fulani aliniambia kwamba kulikuwa na mwangwi, kwa sababu dari namna hiyo. Je! ni afadhali nikisimama nyuma namna *hii?* Ni hivyo? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] La. Inabidi nisonge karibu. Hivyo ni afadhali? ["Ndiyo."] Vema. Hilo ni jema. Vema.

33 Sasa tunataka kugeukia kwenye Maandiko, katika Yohana Mtakatifu 12, na kifungu cha 20, na nisome kutoka hapa.

> Sasa *palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:*
>
> *Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

34 Sasa hilo ni swali kwelikweli, na ni shauku kubwa. Na sasa, kwa dakika zingine ishirini au thelathini, hebu tusikilize kwa makini sana sasa, na ndipo haitakuwa siri kwako.

35 Sasa, mimi ni muumini mkubwa katika kile Neno la Mungu lisemacho. Sasa, ninajua Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Neno. Bali ni. . .ikiwa Yeye atafanya tu yale aliyoahidi katika Neno, hilo litanitosha, ili tu kumwona Yeye. Ndipo ninajua ni kweli, kama Yeye aliliandika katika Neno.

36 Sasa kama Biblia ilisema kwamba, "Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele," sasa Wayunani hawa walikuwa na shauku ile ile, nadhani, ambayo sisi sote tunayo hapa usiku wa leo. Kwani, hakuna mwanadamu, au mtu, aliyewahi kusikia Jina la Yesu Kristo, ila aliye na shauku ya kumwona.

37 Kama ningeuliza wasikilizaji hawa usiku wa leo, nadhani kila mkono ungeinuliwa, "Hivi mngetaka kumwona Yesu?" Hiyo tu ni, unaona, kila mahali. Tunampenda. Vema, basi ninauliza

swali hili, basi ni kwa nini hatuwezi kumwona, ikiwa Biblia ilisema ni Yeye yule jana, leo, na hata milele?

38 Sasa haimaanishi tu kwa njia fulani. Biblia ilisema, "Ni Yeye yule." Sasa kwangu mimi, Biblia ni . . . ama Hiyo si kweli au Hiyo ni sahihi. Sasa, kama hiyo si Neno la Mungu lililovuviwa, basi sijui cha kuamini.

39 Nimekuwa na majaliwa ya kuona aina nyingi, nyingi za dini, moja kwa moja huko—huko—huko Durban.

40 Na huko Bombay, nilipokelewa vizuri alasiri moja katika hekalu la Jaini, ambapo dini kumi na saba mbalimbali za India, kila moja ya hizo ikimkana Yesu Kristo, na kila . . . Nikapokelewa vizuri huko na hizi dini kumi na saba mbalimbali.

41 Ndipo nikaona usiku huo, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu, jinsi ambavyo Mungu aliweka changamoto kwa kila mtu mtakatifu, kila dini, na kila kitu kingine, kwa mtu kipofu aliyesimama jukwaani. Wakati walipoona utambuzi, walidhani ilikuwa ni kuwasiliana kimawazo kwa namna fulani. Ndipo ono likatokea juu ya mwanamume fulani ambaye alikuwa kipofu kwa miaka ishirini, mwabudu jua. Nami nikaona ono kwamba alikuwa anaenda kupona. Ndipo nikampa changamoto kila kasisi wa Kiislamu, kila kasisi wa Budha, kila mtu mtakatifu, Raja, wote, kwamba, "Mtu yeyote atakayekuja hapa na kumpa mtu huyu kuona kwake, nitamwabudu mungu atakayempa kuona kwake. Na yeye alisema atafanya vivyo hivyo." Aliabudu jua.

42 Ndipo nikasema, "Nini, nyinyi mtafanya nini? Nyinyi Waislamu mtafanya nini na yeye? Ungesema, 'Aliabudu ki—kiumbe badala ya Muumba.'" Nikasema, "Ningesema 'amina' kwa hiyo. Lakini hata hivyo hapana budi kuwepo na mtu mmoja sahihi na huyo mwingine makosani." Nikasema, "Ungefanya nini? Ungemfanya yeye Mwislamu. Budha angefanya mwabuduo wa Budha, na kadhalika." Nikasema, "Ungefanya nini? Ungebadilisha tu nia yake. Ungebadilisha tu njia yake ya kuwazia."

43 Nikasema, "Tunalo jambo lilo hilo Marekani. Wamethodisti wote wanataka Wabaptisti kuwa Wamethodisti. Na ndipo Wapresbiteri wanawataka wote wawe Presbiteri. Na—na Umoja unawataka wawe Uwili. Na uwili unawataka wawe . . . Loo, jamani! Ni kitu gani? Ni badiliko la mawazo. Lazima kuwe na kitu halisi mahali fulani. Unaona, kitu fulani hakina budi kuwa sahihi, na kitu fulani si sahihi."

44 Nikasema, "Sasa hebu Mungu wa uumbaji arejeshe kuona kwake, mbele hapa ya watu nusu milioni. Na yeye akasema, mungu yule atakayempa kuona kwake, atamtumikia." Nami nikasema, "Nitakuwa mwanafunzi wa mtu yule anayekuja na kumpa kuona kwake."

45 Hao ndio waliokuwa watu laki tano wanyamavu kuliko wote uliowahi kusikia. Hakuna mtu. Nisingetoa hiyo changamoto kama sikuwa nimeona ono. Sasa, kulikuwa na mashahidi laki tano wa hilo.

46 Ndipo nikasema, "Kwa nini msije? Kwa sababu hamwezi kufanya hivyo." Tena nikasema, "Nyinyi, nyinyi Waislamu, mnadai dini ya Kiislamu kuwa ndiyo kubwa kuliko zote katika taifa," na nikasema, "na ambayo huenda ikawa, kwa idadi; na Budha, na kadhalika. Lakini kwa hakika kuna kuhani fulani anayeweza kuja na kuikubali changamoto hii." Hakuna aliyekuja.

47 Nikasema, "Sababu hamji, ni kwa kuwa hamwezi. Wala na mimi siwezi. Lakini Mungu wa Mbinguni, amemfufua Yesu Kristo, ambaye mimi ni shahidi Wake usiku wa leo, kwamba nimeona ono kwamba mtu huyu anaenda kupokea kuona kwake. Kama hatapokea, basi mimi ni nabii wa uwongo, na mnifukuze kutoka kwa nchi yenu. Lakini kama Yeye akilifanya, basi unawajibika, mbele za makasisi wako na kila kitu, kushuhudia kwamba Yeye kwa kweli ni Mwana wa Mungu, na Mwokozi wa ulimwengu." Kila mtu alinyamaza.

48 Nikamleta mtu huyo kipofu; nikamkumbatia. Nikasema, "Bwana Yesu, kulingana na ono lisiloweza kushindwa, ninakuomba Wewe umpe mtu huyu kuona kwake." Ndipo akaanza kupiga mayowe. Naye meya wa mji alikuwa ameketi pale, ndipo akakimbia na kumshika ghafla. Angeweza kuona vizuri kama nilivyoweza.

49 Basi walikuwa na wanamgambo wa karibu, loo, mamia ya askari, wasingeweza kuwazuia watu. Walikimbia juu ya askari hao, wakakimbia chini ya miguu yao na fimbo, waliyokuwa wakijaribu kuwazuia watu nyuma. Wakati nilipofika kwenye gari na kuondoka, karibu sikuwa na mavazi, hakuna viatu miguuni mwangu, akikimbilia viatu, na kukimbilia koti na kila kitu, akimwonea Mungu njaa na kiu.

50 Lakini Mungu wa Eliya angali anaishi leo, na Yeye ni Mungu tu kadiri Yeye alivyowahi kuwa.

51 Sasa waanzilishi wote wa dini. Akisimama huko kwenye kaburi la Mohammed, amekuwepo farasi mweupe, ambaye amekuwa akisimama huko kwa miaka elfu mbili. Wamebadilisha walinzi yapata kila saa nne au sita, nao wanamtarajia Muhammed kufufuka na—na kusafiri kuzunguka ulimwengu. Mnajua, ninii...na yeye aliandika kitabu cha Koran, na kadhalika. Lakini, loo, Buddha, yapata miaka elfu mbili mia tatu iliyopita, alikuwa m—mtu, mtu wa kidini huko—huko Japan, na kadhalika. Na dini hizi zote, kila mmoja wa waanzilishi wao amekufa na yumo kaburini.

52 Bali Ukristo, baada ya ujuzi wa ulimwenguni kote, Ukristo ndiyo dini ya pekee ya kweli. Ndiyo ya pekee iwezayo kuonyesha

kaburi tupu. Ndiyo ya pekee ambayo mwanzilishi wao, mtu yeyote, na hakuna mtu kama Yeye, aliyewahi kusimama juu ya nchi na kusema, “Ninao uwezo kuweka chini uhai Wangu na kuutwaa tena. Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi. Asiyeamini hataniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi. Kwa kuwa Mimi,” Mimi ni kiwakilishi nafsi, “Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu, hata ukamilifu.” Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele!

53 Sasa tunafikia wazo. Sasa kama Yeye ni yule yule, Yeye hajafa. Amefufuka kwa wafu, na Yeye aliahidi kwamba waaminio Wake wangemwona Yeye, kote hadi mwisho. Moja kwa moja hadi ukamilifu, kwamba wangemwona Yeye, sasa, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

54 Watu wengi ambao nimezungumza nao, kasema, “Vema, kwa njia fulani Yeye ni yule yule.”

Biblia haikusema, “kwa njia fulani.” Ilisema, “Ni Yeye yule.”

55 Na ikiwa tunaona njaa kumwona Yeye, pamoja na shauku ile ile ambayo Wayunani hawa walikuwa nayo. Walikuwa wamesikia kumhusu Yeye, walikuja na wakapata kumwona, kupitia kwa hisani ya mmoja wa wanafunzi Wake. Vema, hivi hatuwezi kufanya vivyo hivyo, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.”

56 Sasa, tunaweza kuzungumza kuhusu ufufuo, tunaweza kuuzungumzia. Lakini ikiwa si uhalisia, inakuwa tu ha—hadithi ya kubuni, ni masimulizi. Bali kama imethibitishwa kuwa ni Kweli, basi sisi ni miongoni mwa watu wenye furaha kuliko wote, na mimi nina furaha kuwa pamoja nao.

57 Sasa, ikiwa—ikiwa Yesu Kristo atajitokeza mbele zetu, usiku wa leo, na tunaweza kuona kwa masharti yaliyotolewa na Mungu, na kwa matendo yenyewe ya Utu Wake, kwamba Yeye yupo hapa, basi tunapaswa angalau kumkubali, kumkaribisha Yeye. Sasa, hilo ni tamshi kubwa, bali tunaye Mungu mkubwa mashuhuri ambaye hutimiza kila moja ya Maneno Yake.

58 Basi tukipata chochote katika Biblia, ifunge nafsi yako kwa hicho. Hiyo ni Kweli. Dumu tu moja kwa moja na kile alichoahidi Mungu, Mungu atatimiza.

59 Kama sisi ni watoto wa Ibrahimu, tunaamini mambo hayo. Ibrahimu, kinyume na hali kubwa, aliviita vitu visivyokuwapo, kana kwamba vilikuwapo, kwa sababu aliamini kwamba Mungu aliweza kutimiza Neno Lake. Na sisi tunajiita watoto wa Ibrahimu. Ibrahimu aliingojea ahadi kwa miaka ishirini na mitano. Badala ya kuwa dhaifu, alizidi kuwa na nguvu. Na jinsi inavyoonekana tofauti leo hii na Uzao Wake wa kifalme.

60 Sasa, uzao halisi wa Ibrahimu ni—ulikuwa ni Isaka, tunatambua hilo, ambao ulitokea Myahudi, ambao ni wa kimwili.

61 Lakini Uzao ambao Mungu alikuwa anatolea ahadi, ulikuwa ni Uzao wa Ibrahimu, imani aliyokuwa nayo katika Mungu. Ambao, kupitia Yesu Kristo, Ambaye ni Neno Lake, tunafanyika warithi pamoja na Yeye. Basi kanisa hili, usiku wa leo, la wasafiri wa siku hii, kabisa ni Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, wakiwa na imani halisi.

62 Sasa, kama ningewauliza Wamethodisti, "Je! mnaamini hilo?" "Naam." "Mnaamini Yeye yuko pamoja nanyi?" "Naam." Wabaptisti, Presbiteri, Lutheri, Pentekoste, kadhalika, kila mtu angesema vile vile.

63 Lakini sasa tungemtafuta Yeye kwa njia gani? Ni mtu wa namna gani ambaye tungemtafuta, iwapo tulitaka kuona kama Yeye alikuwa ni yule yule? Kama Yeye angekuwa hapa Arkansas, usiku wa leo, katika maskani hii, ni mtu wa namna gani ambaye tungemtafuta?

64 Sisi, sisi tungemtafuta mtu ambaye, vema, labda aliye na joho refu, na ndevu usoni mwake, na makovu ya msumari mkononi mwake, na alama za miiba kwenye pa—paji lake? Kama ungetafuta mtu kama huyo, mnafiki yeyote angeweza kukudanganya juu ya hilo. Hiyo ni kweli, uigaji. Mtu angeweza kuchora kwa rangi makovu mikononi mwake, na hata angeweza kujidunga mwenyewe na miiba na kufanya makovu, lakini mwigaji yeyote angeweza kufanya hilo.

65 Lakini basi kama hatukuwa tukimtafuta mtu wa namna hiyo, si kwa ajili ya vazi lake wala kile kilicho kimo chake. Kwa sababu, kama Yeye alikuwa hapa, Yeye angevalia kama sisi. Hakukuwa na tofauti yoyote. Alivalia na kutembea miongoni mwa watu sawa tu na jinsi watu walivyokuwa. Yeye kamwe hakuvalia kama makasisi wa siku hiyo. Alivaa tu mavazi ya kawaida ya mtaani. Kwa hiyo Yeye angevalia tu kawaida, labda akiwa na suti, na kadhalika, kama mtu yeyote mwingine leo angevalia. Kama mtu anayefanya kazi, ama m—mfanyabiashara, ama chochote zaidi, hiyo ingekuwa ndiyo jinsi Yeye angevalia. Kwa hiyo kamwe humjui kwa njia hiyo. Usingeweza kumjua Yeye kwa umbo la kimo, kama alikuwa mrefu, mwembamba, mfupi, mnene; au, sisi, hatujui, kwa hiyo usingeweza kujua.

66 Bali ninasema kile Yeye angekuwa, kama Yeye alikuwa hapa leo hii, Yeye angekuwa ni Neno la Mungu. Hilo hasa ndilo alilokuwa Yeye, na angali hilo. Yeye ni Neno, sio tu Neno lililoandikwa (Yeye ni Neno lililoandikwa), bali dhihirisho la Neno lililoandikwa. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Mungu, Neno, alidhihirishwa katika mwili, ili kwamba Maneno Yake yaweze kunenwa kupitia midomo ya mwanadamu na kufanyika Neno.

Basi yeye alidhihirishwa katika mwili, huyo alikuwa ni Yesu Kristo, Mungu, Imanueli.

Sasa unasema, "Je! Yeye ni Neno?"

67 Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, inatwambia, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa katikati yetu."

68 Ni nini yaliyokuwa baadhi ya mambo ambayo Yeye angefanya? Tunaona, katika Waebrania, mlango wa 4 na kifungu cha 12, Biblia ilisema kwamba, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na ni mtambuzi wa mawazo ya moyo." Neno ndilo. Kwa hiyo Neno ni mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Hilo lingemstahilisha Yesu, kabisa, kuwa ni Neno. Yeye alijua mawazo yaliyokuwa moyoni mwao. Waebrania 4:12.

69 Sasa kama tulitaka kumtambulisha Yeye, je! tungemtarajia kuwa namna fulani ya Daktari wa Elimu ya Kiungu? Hakuna rekodi ya Yeye kuwahi kuwa shuleni.

70 Je! tungemtambulisha na dhehebu lolote? Alikuja katika wakati ambapo kulikuwa na madhehebu mengi, lakini Yeye hakujihusisha Mwenyewe na lolote la hayo. Kwa hiyo Yeye. . . Hatungeweza kusema kwamba Yeye alikuwa ni Farisayo, au Sadukayo, ama ka—kadhalika. Tusingeweza kumtambulisha Yeye na dhehebu lolote.

71 Alikuja kwa ajili ya watu. Mungu, akiwa ni Mungu wa wote, Yeye ni Mungu wa maumbile yote. Alikufa ili kuwaokoa wenye dhambi katika kila kanisa, ku—kumponya kila mtu mgonjwa. Alikuja kuwakubali wale ambao wangemkubali Yeye.

72 Hivyo ndivyo vile Yeye alivyo hapa usiku wa leo, kuwaponya wale ambao wanamkubali, kuwaokoa wale ambao watamkubali. Yeye huja katika umbo lile lile, katika njia ile ile.

73 Kama akija, itambidi kuja katika utambulisho wa Kimaandiko. Ikiwa Yeye hakujitambulisha Mwenyewe. . . Hakuna mahali tungeweza kupata katika Biblia, katika Agano la Kale, ila kwamba Yeye alijitambulisha Mwenyewe sawa na Maandiko, sana hata Yeye alisema, "Nani, ni yupi kati yenu awezaye kunihukumu Mimi kwamba nina dhambi?"

74 Sasa, sisi sote tunajua kwamba *dhambi* ni, "kutokuamini." "Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari." Sasa, dhambi ni sifa ya kutokuamini. Kuvuta sigara si dhambi. Kuiba si dhambi. Kusema uongo si dhambi. Kufanya uzinzi si dhambi.

"Ni kitu gani basi?" ungesema.

75 Ni sifa za kutokuamini. Kama ulikuwa ni mwaminio, usingefanya mambo hayo. Sababu ya wewe kuyafanya, inathibitisha kwamba wewe ni asiyeamini. Unaona? Vipo

vikundi viwili tu, hivyo ni, ama wewe ni mwaminio au asiyeamini.

76 Na jinsi, daima imenikanganya, kwamba mtu anaweza kudai kuwa na Roho Mtakatifu ndani yake, na alikane Neno la Mungu kuwa ni kweli. Wakati, Roho Mtakatifu Mwenyewe aliliandika Neno la Mungu. Na nyinyi mnajua Yeye asingeweza kujiita Mwenyewe uwongo. Kwa hiyo Yeye aliandika Maandiko, na Yeye husimama kwa Maandiko, na Mungu huyaangalia Hayo, kuthibitisha Hayo.

77 Kwa hiyo hebu turudi tu nyuma na tuone kile Yeye alichokuwa, ikiwa tunataka kujua kama Yeye ni yule yule leo. Njia ya pekee ya kweli ya kutafuta kujua, ni kutafuta kujua kile Yeye alicho leo hii, ni kurudi nyuma na kutafuta kujua kile Yeye alichokuwa jana, ndipo tunajua kile Yeye atakachokuwa leo. Je! hiyo ni nzuri vya kutosha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kama tunaweza kupata kile Yeye alichokuwa jana!

78 Bila shaka, tunaweza kuanza nyuma na hadithi ndefu. Sitaki kuwaweka muda mrefu, maana inawabidi kuwa hapa kesho, na tunataka kufanyiza mstari wa maombi, ila ninawatakeni kuchukua hili kabisa sasa na kusikiliza kwa makini. Kama tunaweza tu kurudi nyuma na kuona kile Yeye alichokuwa jana, tunaweza kujua basi kile Yeye alicho leo, kwa sababu Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

79 Sababu nilikuwa nikifungua kurasa hizo, ilikuwa ni kutafuta hapa nyuma ku. . .Ninaanza na ninasoma Yohana Mtakatifu 12:20, hebu tuendelee tu katika Yohana Mtakatifu. Tunaweza kuichukua mahali popote katika Maandiko ambayo mnataka, kwa sababu Kitabu chote ni ushuhuda wa Yesu Kristo. Ni ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. Hakuna kitu kinachoweza kuongezwa kwa Hicho au kuondolewa Kwacho. Hicho ndicho alicho Yeye. Yeye ni Imanueli, na hilo—hilo latosha; haijalishi kile tunachojaribu kumfanya Yeye, kitu kingine, ama nabii, ama—ama kitu kama hicho. Yeye alikuwa ni nabii; Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii. Yeye ni Mungu-nabii. Lakini Yeye alikuwa—Yeye alikuwa zaidi ya hiyo. Alikuwa ni Imanueli; si tu mtu mwema, mwalimu, mwanafalsafa. Yeye alikuwa yote hayo, pia, na pamoja na hiyo. Unaona?

80 Sasa katika Yohana Mtakatifu, wa kwanza, tutaanza usiku wa leo, na labda kesho tuchukue kidogo, Kitabu kingine. Hebu tuanze katika Yohana Mtakatifu 1. Tunaona. . .Sisi sote tunajua kuzaliwa Kwake na bikira, kwamba jinsi Mungu alivyomtia bikira uvuli, na kuumba seli ya Damu iliyomzaa huyo Mwana, Kristo Yesu. Na katika ukingo wa Yordani, wakati Mungu aliposhuka katika umbo la Nuru, ama hua, hakuna aliyeiona hiyo ila Yohana. Watu hao wote waliosimama karibu, hawakuiona Hiyo. Hakuna aliyeona Hiyo ila Yohana. Alikuwa

ndiye wa pekee aliyekuwa akitazamia Hiyo, kwa hiyo Mungu alikuwa amemwambia kuwa angeiona Hiyo.

81 Unaona tu kile unachotazamia. Ukija hapa usiku wa leo ukimtazamia Kristo, utamwona. Ukija ili kukosoa, utakuwa na mengi, mengi mkononi mwako kukosoa. Inategemea kile ambacho unatafuta.

82 Yohana alisema, “Yeye aliyeniambia huko nyikani kuenda kubatiza kwa maji, alisema yule ambaye ‘nitaona Roho akishuka juu yake na kutulia, Huyo ndiye Yule ambaye atabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.’” Yohana alishuhudia, kasema, “Niliona Roho wa Mungu akishuka kutoka Mbinguni, kama hua, na Huyo akaenda juu Yake.” Ndipo basi Yeye akapelekwa nyikani, na majaribu. Akatoka nyikani, na punde, tunaona, anaombea wagonjwa.

83 Sasa, mnaona, jambo la kwanza, Roho wa Mungu alikuja juu Yake kabla ya huduma Yake, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kusema, “Si Mimi nifanyaye kazi, ni Baba anayekaa ndani Yangu. Yeye hufanya kazi.” Sasa tunaona kwamba huduma Yake ilianza, akaanza kuwaponya wagonjwa, kwa—kwa maombi.

84 Sasa Mungu huponya kwa njia nyingi. Daktari fulani aliniuliza, si muda mrefu uliopita, kasema, “Ni nini maoni yako kuhusu dawa, Ndugu Branham?”

85 Nikasema, “Vema, Mungu Ndiye wa pekee awezaye kuponya, bwana.” Nikasema, “Biblia haisemi uwongo, na Biblia ilisema, ‘Mimi ndimi Bwana, aponyaye magonjwa yenu yote.’” Tena nikasema, “Biblia haiwezi kusema uwongo.” Nikasema, “Mungu huponya kwa dawa. Mungu huponya kwa upendo. Mungu huponya kwa ufahamu. Mungu huponya kwa utunzaji. Mungu huponya kwa maombi. Mungu huponya kwa miujiza. Kitu chote, Mungu huponya. Ni hayo tu, yote yaliyoko kwa hilo, Yeye ndiye mponya.”

86 Hatujapata dawa iwezayo kuumba, na kuumba seli katika mkono wako, kuponya; kuumba katika mwili wako, kuponya. Tunaweza kutoa jino, tunaweza kukata na kuondoa kidole tumbo, au kuondoa kibofu nyongo, lakini ni nani aliyeponya? Mungu. Hakuna dawa itakayojenga tishu, Mungu pekee. Uhai hujenga tishu. Mungu ndiye mponyaji wa pekee, na tulikuwa tunazungumzia hilo.

87 Basi tunaona sasa, kwamba Yesu alienenda akiwaponya wagonjwa. Na kulikuwa na mmoja wa wanafunzi Wake jina lake Andrea.

88 Na mimi ninataka kufanya huu kuwa mchezo wa kuigiza kwa sababu wapo watoto wameketi hapa, na msichana mdogo mgonjwa amelala hapo chini. Ninataka auelewe.

89 Mnajua, Andrea alikuwa ni kaka yake Simoni, ambaye baadaye aliitwa Petro. Basi Andrea alikuwa amekuwa m—mfuasi wa Yohana. Na Yohana alikuwa ametangaza kwamba kulikuwa kunakuja Masihi, naye alikuwa na hakika kwamba ingekuwa katika kizazi chake. Hiyo ndiyo sababu yeye kamwe hakuenda shule zozote wala seminari. Kazi yake ilikuwa muhimu sana.

90 Mbona, mnajua, kama kuhani angeweza kufahamu kuwa yeye alikuwa awe ndiye wa kutangaza kuzaliwa. . . ama kuja kwa Masihi, na kumtambulisha Yeye kwa ulimwengu, mbona, wangesema, "Sasa, sasa, Daktari Yohana, hivi hujisikii kwamba Ndugu *Nanii* hapa, hufikirii kwamba amehitimu kuwa Masihi? Mbona, hebu mwangalie, yeye—yeye—yeye anao usuli mzuri. Unajua unajua hilo, huyo ndiye Masihi. Kwa nini usiende na kuambia ulimwengu?"

91 Bali, unaona, kazi yake ilikuwa muhimu zaidi ya kushawishiwa na binadamu. Alienda nyikani na kungojea katika seminari ya mafunzo ya Mungu, hata Mungu akamwambia, "Yule Ambaye utamwona Roho akishuka juu yake, huyo Ndiye wa kutangaza, Masihi." Unaona?

92 Sasa tunakuta kwamba Andrea alikuwa ameamini hilo, hapana shaka alikuwa amerudi na kumwambia Simoni kuhusu hilo, mara nyingi. Lakini Simoni, akiwa kwa namna fulani ni kichwa ngumu, vile sisi. . . Samahani tamshi hili; natumai halisikiki la kukufuru. Lakini yeye, kidogo akiwa ni kichwa ngumu, kama tungeliita leo hii, "Loo, endelea, kama unataka kusikiza hilo." Basi siku moja alikuja na kumwambia kwamba alikuwa amempata Masihi, na ilikuwa vigumu kwake kuamini hilo.

93 Basi ninaweza kumwona Andrea akimleta Simoni huku juu sasa mbele za Bwana Yesu. Mara ya kwanza alipopata kumwona Huyo. Yesu alikuwa tu amerudi kutoka nyikani. Huduma Yake ilikuwa inaanza, sasa Yeye ilibidi atambulishwe. Basi punde tu Simoni alipotembea kuingia katika Uwepo wa Bwana Yesu, Yesu alimtazama na kusema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona."

94 Sasa mara moja tunaona kwamba Simoni aliamini. Yeye basi alikuwa na jina la Petro. Ni kwa nini aliamini hilo?

95 Nilisoma hadithi ya baba yake, Yona, alikuwa mtu mashuhuri wa—wa maombi. Alikuwa amewalea wavulana wake ku—kumwamini Mungu. Na kila siku kazi yao ilikuwa ni uvuvi, mara nyingi sana wangepiga magoti yao na kuomba ili Mungu awape mshiko mzuri wa samaki ili waweze kulipa madeni yao na kupata riziki ya siku hiyo.

96 Na kabla hajafa, maskini jamaa huyo aliketi demani mwa chombo chake siku moja, na akawaambia wavulana hao, akasema, "Wanangu, sisi ni Waebrania, na tunaamini

kwamba kulikuwa na Masihi ajaye. Na mimi daima nimetumaini kwamba ningeishi kuona siku ya kumwona Masihi akitembea duniani kwa miguu Yake. Basi mimi. . .ila nadhani sitaishi siku hiyo, kwa sababu mimi ni mkongwe sasa na sina budi kuondoka. Lakini, wavulana, Shetani hatamwacha Masihi huyo ainuke pasipo na masihi wengi bandia kwanza. Kwa hiyo ninawatakeni enyi wavulana mkumbuke, msishangazwe na ma—mambo mengi yatakayotokea. Ila ninawatakeni enyi wavulana mfunzwe. Kumbukeni, kwamba tuna hili: Masihi, wakati Yeye atakapokuja, Yeye itabidi atambulishwe Kimaandiko na Mungu, kabla ya Yeye kuwa ni Masihi." Tunahitaji baba wengi kama huyo leo hii!

97 "Yeye itabidi awe Kimaandiko ni Masihi. Na sasa tumemfuata Musa, nabii mkuu aliyewaongoza watu wetu kutoka Misri, na tumesikiliza mafundisho yake. Na sisi—sisi tunajua kwamba—kwamba Musa alikuwa sahihi. Na katika Kumbukumbu la Torati, mlango wa 18, Musa alituambia kwamba, 'Masihi; Bwana Mungu wenu atawainulia nabii aliye kama mimi, na wao hawana budi kumsikia Yeye.'"

98 Sasa, Israeli daima walifunzwa kuwaamini manabii tu. Nyinyi walimu wa Biblia mnajua hilo. Naye nabii angeweza tu kutambulishwa, nabii, kwamba wakati alipotabiri na kile alichosema kikatimia. Biblia ilisema, "Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitanena naye, nijitambulishe Mwenyewe kwake, katika maono na ndoto. Na kile asemacho kinatimia, basi msikieni. Lakini kisipotimia, msimwogope." Hilo hilo, hilo ndilo Yeye alilomwambia Musa kuwaambia watu, na huo ulikuwa ndio utambulisho wao wa Kimaandiko kwamba Masihi angekuwa ni nabii.

99 Sasa mtu yeyote anajua kwamba Neno la Bwana huja kwa nabii; si kwa kasisi, bali kwa nabii. Biblia ilisema hivyo. Neno la Bwana lilimjia nabii. Na sisi tunajua, kama ni Neno la Bwana, na nabii ni wa kweli, basi maneno yake ni kweli, basi maneno yake yanatimia. Na huo ndio utambulisho wake, huo, kwanza, ni Neno. Na, kwanza, Mungu ni Neno. Ndipo basi akinena neno, nalo linatimia, basi hiyo inaonyesha kwamba Mungu amemwandaa mtu huyo Kiungu.

100 Sasa basi tukiwa na hilo niani, huenda waliinua kila namna ya misisimko na kila kitu kingine ulimwenguni, hao wanafunzi wa Biblia wasingeweza kuamini hilo, kwa sababu Masihi ilibidi awe ni nabii. Na wao hawakuwa wamekuwa na nabii kwa miaka mia nne. Malaki alikuwa ndiye nabii wa mwisho. Hakuna nabii.

101 Basi hapa anakuja Simoni, akiwa na funzo kama hilo, katika uwepo wa Mtu ambaye kaka yake alimwamini kwa dhati kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Na punde tu anapotembea kuingia katika Uwepo Wake, si tu kwamba Yeye alimjua kuwa

ni nani, Yeye alimjua yule maskini baba yake mtauwa, Yona. Si ajabu iliondoa ugumu ndani yake. Alijua huo ulikuwa ndio utambulisho wa kweli wa Masihi. "Lako, jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona."

102 Na mtu asiyekuwa na elimu hata hakuweza kutia sahihi jina lake, tunaambiwa; Biblia ilisema, katika Kitabu cha Matendo ya mitume, mlango wa 3, kwamba, "alikuwa asiye na elimu wala maarifa." Lakini ilimpendeza Mungu kumfanya kiongozi wa kanisa huko Yerusalemu, na kumpa funguo za Ufalme. Maana, wakati mbegu hiyo teule iliyolala pale ndani ya huyo maskini mvua samaki, na wakati Nuru ilipoimulika, upesi ilitambua kwamba huyo alikuwa ni Masihi.

103 Sasa hiyo ilithibitisha hapo, kwamba mtu huyo alijua, ilithibitisha kwamba mbegu hiyo ilikuwa imelala pale. Jina lake lilikuwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo tangu msingi wa ulimwengu, wakati Mwana-kondoo alipouawa katika mawazo ya Mungu Mwenyewe. Na punde tu Nuru hiyo ilipoimulika hiyo, upesi ikawa hai na kutambua hiyo kuwa ndiye Masihi.

104 Kulikuwapo mmoja aliyesimama hapo jina lake Filipo, naye aliona hili, upesi ikaja niani mwake. "Hiyo kwa kweli ni Yeye, kwa kuwa ninajua Maandiko. Mtu huyo hakuwa amemwona mtu huyo hapo kabla, basi Yeye angejuaje kwamba alikuwa ni nani? Huyo ni Nabii."

105 Alitoka kwenda kumtafuta rafiki yake ambaye alikuwa akifanya masomo ya Biblia pamoja naye, tangu akiwa mvulana. Jina lake lilikuwa Nathanaeli. Ni maili kumi na tano kutoka mahali walipokuwa wakihubiri, kuzunguka mlima, hadi mahali Nathanaeli alipokuwa na shamba la mzeituni. Ninaweza kumwazia Filipo akienda zake, akiruka na kupaza sauti. Alikuwa amepata kitu kilichokuwa halisi.

106 Loo, jinsi Hicho kinapaswa kuitia moto mioyo yetu, kuzunguka vilima, kuvuka mbuga, chini kupitia makondeni, chini kwenye vichochoro, kuvuka mtaani, kote kupitia taifa, mahali fulani.

107 Alipata kitu. Na alikuwa na rafiki. Masomo ya Biblia, hapo kabla, yalikuwa yamethibitisha kwamba huyu Masihi wa Kimaandiko angekuwa Nabii. Hakuna manabii kwa miaka mia nne.

108 Wakati anapofikia mahali hapo, anamkuta Nathanaeli chini ya mti, akiomba. Na labda alisimama kwa dakika chache, kungojea, kama Mkristo mwungwana, kungojea mpaka alipomaliza maombi yake. Basi wakati aliposimama, labda alikuwa akipangusa vumbi kutoka kwenye joho lake, Filipo huenda alisema upesi, "Nathanaeli!"

Ndipo akaja karibu, kasema, "Filipo, mwenzangu, nina furaha kukuona!"

109 Na labda mazungumzo yalikuwa kitu kama hiki. Unaona, hakuwa na wakati wa kusema, "Mizeituni inaendeleaje?" Ama, "Mke na mtoto wako namna gani?" Unaona, ujumbe ulikuwa wa dharura. Alikuwa ameona kitu fulani. Alikuwa ameona Maandiko yakitambulishwa, Masihi, na hicho ndicho walichokuwa wametazamia kwa miaka na miaka na miaka. Akasema, "Njoo, umwone Yule tuliyempata! Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu, njoo, umwone Huyo!" Ujumbe ulikuwa wa dharura.

110 Nawaambieni, ndugu zangu, laiti tungaliweza kupata shauku ya aina hiyo, kwamba Ujumbe wetu ni wa dharura sana. Hatuna muda kwa ajili ya upumbavu. Hebu tuwapelekee watu Ujumbe, watu ambao wametokwa jasho kupitia mateso, ndio watoto wa baba zetu waliosimama mitaani, wakiwa na—wakiwa na tari mkononi mwao, na wangekula mahindi kutoka kwenye gari la moshi, kuunga mkono hii Njia Kuu, Injili hii. Na sasa tunamwona Kristo miongoni mwetu, hebu tuende ulimwenguni na Hiyo, upesi tuwezavyo, na tumpate.

Kasema, "Njoo, mwone Yule tuliyempata."

111 Sasa tunaona kwamba Nathanaeli alikuwa ni mwanatheolojia kwelikweli, nami ninaweza kumwazia akimwambia Filipo, "Sasa ngoja tu kidogo, Filipo, umepatwa na kichaa cha aina gani?" Unajua, mazungumzo hayo yangali yanaendelea leo hii, unaona. "Ulipatwa na kichaa gani?" Kuharibikiwa akili mahali fulani, mwajua. "Ni—ninakujua kuwa na akili timamu, mtu wa maana, na hapa unakuja ukikimbia na kuniambia kwamba Masihi yuko hapa duniani?"

112 Alipaswa awe amezungumza na mamajusi. Mwajua, mamajusi walikuwa huko juu Babeli. Walikuwa ni Wayahudi huko juu wakisomea unajimu. Ndipo walipoona hizo nyota tatu zikipangana, hiyo ilikuwa ni ishara, ishara ya kale ya Kiebrania, kwamba wakati nyota hizo tatu zikipangana, Masihi alikuwa duniani. Walikuja, wakipaza sauti, "Yuko wapi Yeye, aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tuliona Nyota Yake na tumekuja kumsujudia."

113 Lakini, Filipo, hili. Hawakuwa na njia mbalimbali za matangazo kama televisheni, redio na magazeti, na vitu katika siku hizo, na wao kamwe hawangechapisha chochote namna hiyo hata hivyo. Kwa hiyo kitu cha kwanza tunajua, tunaona Filipo na Nathanaeli wakizungumza, "Vema," alisema, "njoo."

114 Akasema, "Tazama, je! kitu chochote chema kinaweza kutoka kwenye kundi la watakatifu wa-. . ." ama samahani, "kundi la watu namna hiyo, kutoka Nazareti?"

115 Vema, mnajua kile ninachowazia? Filipo alimpa jibu zuri kuliko yote mtu yeyote angeweza kumpa mtu. Hakujaribu kulieleza. Hakujaribu kuingia katika uchambuzi wake. Yeye alisema tu, "Njoo uone. Njoo, ujionee mwenyewe. Chomeka

hicho chuo chini ya mkono wako, cha Kumbukumbu la Torati 18, na uje unifuate ndipo tutaona."

116 Hebu tuchukue mazungumzo yao walipokuwa wanatembea. Unaona, iliwabidi kufika huko, siku moja, na kurudi siku iliyofuata, maili kumi na tano. Kwa hiyo wakiwa njiani, wakizunguka, ninaweza kumsikia Filipo akisema, "Sasa angalia, Nathanaeli, masomo mengi ya Biblia kama tuliyokuwa nayo, tunaamini kwa dhati kwamba Masihi anapaswa awe ni Mungu-Nabii, maana Musa alisema hivyo. Na sisi tulimfuata Musa, na tulipaswa kumfuata mpaka Nabii huyu alipofika. Ndipo wakati Nabii huyu alipokuja jukwaani, basi Yeye angetwambia njia ya maisha, tangu hapo na kuendelea. Basi ikiwa . . . Unajua, wasiomwamini Yeye watakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa watu, tusipomwamini Yeye."

"Vema, unajuaje kwamba jamaa huyu ni Nabii?"

117 Kasema, "Je! unamkumbuka yule mvuvi mzee huko chini, ambaye ulimnunulia wale samaki siku ile, kutoka kwake, na yeye hakuwa na elimu ya kutosha kutia sahihi jina lake kwenye risiti?"

"Naam, ninamkumbuka. Loo, jina lake lilikuwa Simoni. Naam."

118 "Ndugu yake, Andrea, amekuwa akihudhuria mkutano wa Yohana. Basi wakati alipoona tangazo, na kusikia tangazo la Yohana, akisema, 'Huyu alikuwa ndiye Masihi.' Na, Yohana, tunajua alikuwa nabii, kwa hiyo asingeweza kusema lolote la uwongo. Alitangaza, 'Huyo ndiye Masihi,' na kwa hiyo alisema aliona ishara juu Yake. Na yeye alimleta ndugu yake jana. Ndipo mara alipotembea kuingia katika Uwepo Wake, Yeye alisema, 'Jina lako ni Simoni, na wewe ni mwana wa Yona.' Mbona, isingenishangaza kama Yeye hataniambia kuwa wewe ni nani, wakati ukifika huko," angesema.

119 "Loo," akasema, "sasa ngoja kidogo, ngoja kidogo! Inanibidi kujionea hilo mwenyewe. I—i—inanibidi kuona hilo."

120 Kwa hiyo tunaona hapa, siku iliyofuata, kile kinachofanyika. Waliwasili, umati mkubwa wa watu umesimama. Yesu labda alikuwa akizungumza. Labda walikuwa wameketi, wengi wao, labda walikuwa wamesimama; sijui. Lakini, hata hivyo, Filipo alikuja, na akamleta Nathanaeli, na wakati Yesu alipogeuka na kumwangalia, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli, Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake."

121 Mbona, ilimshtua sana mtu huyo! Akasema, "Rabi, namna gani, Wewe ulijuaje chochote kunihusu? Si—si—si—sikujui Wewe. Na Wewe hujawahi kuniona, na mimi sijawahi kukuona. Namna gani, Wewe ungewezaje kujua chochote kunihusu mimi?"

122 Akasema, "Vema, kabla Filipo hajakuita, ulikuwa chini ya mti. Nilikuona." Loo, jamani, ni macho ya namna gani! Siku

iliyotangulia, na maili kumi na tano kuzunguka mlima, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona wewe."

123 Je! huyu msomi aliyeelimika, aliyepaswa kuwa, mwana wa Mungu, alijifunza nini? Alijifunza kwamba huo ulikuwa ni utambulisho wa Masihi. Alifanya nini? Hapana shaka alitazama kote na kumwona kuhani wake, na wote wengine, wamesimama. Alikimbia hadi miguuni Pake, akaanguka chini, na kusema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli."

124 Yesu akasema, "Umeamini kwa sababu nimekwambia mambo haya. Sasa utaona mambo makuu zaidi ya haya."

125 Loo, lakini kulikuwa na wengine waliosimama karibu, makuhani, makasisi. Na walijua ingewabidi kutoa hesabu kwa kusanyiko lao, kwa hilo, kwa hiyo iliwabidi kusema jambo. Unajua walichosema? "Mtu huyu ni Beelzebuli. Yeye tu ni mpiga ramli, ama namna fulani ya ibilisi."

126 Ndipo Yesu akageuka na kusema, "Mkisema hayo dhidi ya Mwana wa Adamu, mtasamehewa. Lakini atakapokuja Roho Mtakatifu kufanya jambo lilo hilo; kunena neno moja dhidi Yake, hakutasamehewa katika ulimwengu huu wala—wala katika ulimwengu ujao." Ni mahali pa jinsi gani hilo lingetuweka basi!

127 Sasa tunaona, kote chini, tungeweza kupitia Maandiko. Wao. . .Hebu tuchukue ukurasa mwingine na tugeukie Biblia tena. "Tulikuwa na haja kupitia Samaria," siku moja alipokuwa njiani Mwake kuenda Yeriko. Yeriko ilikuwa chini ya mlima, na Yerusalemu ilikuwa juu ya kilima. Samaria ndiyo njia ya kurudi, ingekuwa ni kama kwenda Ca—California kupitia njia ya—ya Hot. . .kupitia njia ya Little Rock. Ungezunguka huko. Bali Yeye alikuwa na haja kupitia Samaria. Sasa tunaona kwamba, Wasamaria, walitokana na ku—kundi lililochanganyikana la watu.

128 Zipo jamii tatu tu za watu duniani, hizo ni: watu wa Ham, Shem, na Yafethi. Kama tunaamini Biblia, zote zilianza kutokana na watoto wa Nuhu, na hizo ndizo zilitokea ulimwenguni.

129 Na sasa tunakuta kwamba: Myahudi, na Mtaifa, na Msamaria. Petro, akiwa na funguo alizopewa kwenye Pentekoste, aliufungua kwenye Pentekoste, kwa Wayahudi, aliufungua huko chini kwa Wasamaria, na kuufungua kwa Mataifa. Ndipo jamii yote, hizo jamii, zilikuwa zimesikia Injili. Humsikii tena akizitumia hizo funguo, kwa sababu Injili ilikuwa imefunguliwa wote hao. Angalia sasa.

130 Hawa Wasamaria walikuwa nusu Myahudi na Mtaifa. Walimwamini Mungu yule yule ambaye Wayahudi walimwamini, nao walikuwa wanamtazamia Masihi ajaye.

131 Sasa, Masihi ataonekana tu kwa wale wanaomtazamia Yeye. Unaona? Sasa sisi Mataifa hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote, wala hatukumwona yeyote. Hii ndiyo siku yetu.

132 Kwa hiyo Wa—Wasamaria walikuwa wanamtazamia Masihi. Basi ikiwa Masihi alikuwa duniani, anawajibika, kwa watu wa Samaria, kujitambulisha Mwenyewe kama Yeye alivyofanya kwa Wayahudi.

133 Sasa yeyote wetu anajua kwamba Masihi alijitambulisha Mwenyewe kwa kuwa yule nabii ambaye Musa alisema kuwa Mungu angemwinua. Ni wangapi wanaamini hilo, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika.

134 Yeye alikuwa ndiye Nabii. Alitambulisha. Sasa, huyo alikuwa ni Yesu jana. Basi kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, itakuwa ni Yesu leo, jambo lile lile.

135 Sasa tunamwona Yeye akienda juu kwenye mji huu wa Sikari, na—na ilikuwa inaelekea mwendo wa adhuhuri. Nao wanafunzi walienda zao mjini, kununua chakula. Maakuli, ndivyo yanavyoitwa katika Maandiko. Basi walipokuwa wameenda, Yesu alingojea.

136 Kama umewahi kuwa huko, ni namna ya mandhari kama hii; kisima, ama kisima cha mjini, cha umma, nje ya mji. Kingali kinasimama leo. Na watu walikuja na kuchota maji yao, na kurudi ndani ya mji. Na wanayabeba kichwani mwao, majagi. Nao wanawake wanaweza kuweka jagi ya karibu galoni tano kichwani mwao, na kuweka moja juu ya kila nyonga na wanaweza kutembea, wakizungumza na wanawake kama wanawake wawezavyo tu kufanya, na—na kamwe wasimwage hata tone la maji. Si—sioni jinsi wawezavyo kufanya hilo, lakini wao—wao hulifanya, uwekaji sawasawa kikamilifu, wakiongea na kuongea kama kina mama wafanyavyo wanapotembea, huku wamebeba haya majagi, karibu galoni kumi na tano za maji, wakitembea namna hiyo, wakiongea. Na wanawake hawa, kwa sababu . . . Wangali wanafanya jambo lile lile kama walivyofanya wakati huo, nao wanawake hawa wanakuja kisimani kuteka maji yao.

137 Sasa kulikuwako, mwendo wa yapata saa tano au saa sita, kulikuwa na mwanamke mwenye sifa mbaya, kwa namna fulani mnajua ninachomaanisha, mwa—mwanamke kahaba alikuja kisimani kuteka maji, ndipo akaanza kuteremsha m—mtungu wa maji. Wana wi—winchi, na kulabu mbili zinaenda juu ya jagi hili, au ndoo, nao wanaiteremsha ndani ya kisima, nayo inageuka upande wakati ikifika kwenye maji, ndipo wanayavuta maji haya kurudi juu. Naye alikuwa tu anajitayarisha kuteremsha ja—jagi lake chini, wakati alipomsikia mtu fulani, kasema, "Niletee maji ninywe." Ndipo akaangalia, na akamwona M—Myahudi ameketi kuegemea ukuta, mahali mzabibu unaponing'inia juu ya ukuta, na Yeye alikuwa ameketi hapo. Yeye—Yeye hapana

shaka alikuwa ni Mtu mwenye umri wa makamo, au alionekana mwenye umri wa makamo.

138 Nafikiri alionekana mzee kidogo kuliko kile Yeye alichokuwa hasa. Kwa sababu, tunaona katika Yohana Mtakatifu 6, kwamba mazungumzo yalitokea kuhusu maji ya kunywa kwenye. . . nyikani, na kadhalika, na—na jinsi ambavyo walikuwa wanafurahia mkate, ukiwakilisha mana. Ndipo Yesu akasema, "Mimi ndimi ule Mwamba uliokuwa nyikani."

139 Nao wakasema, "Wewe ni Mtu asiyezidi miaka hamsini," unaona, na Yeye alikuwa na miaka thelathini tu. "Wewe ni Mtu asiyezidi miaka hamsini." Uchovu Wake mkuu hapana shaka ulivuruga sehemu Yake ya kibinadamu, na Yeye huenda alikuwa anaingia mvi kidogo, ama kitu fulani. Kasema, "Wewe ni Mtu usiyezidi miaka hamsini, na unasema Wewe 'umemwona Ibrahimu'? Sasa tunajua kwamba Wewe ni mwendawazimu, ama una kichaa."

140 Na Yeye akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Walikuwa tu wanamwangalia mwanadamu. Ilikuwa ni kile kilichokuwa ndani yake kikinena. Na "MIMI NIKO" alikuwa nyikani pamoja na Musa, katika kichaka kilichowaka moto.

141 Basi hapo tunapata kwamba Yeye alionekana kidogo amezeeka. Basi, Yeye, mwanamke alimwona Myahudi mwenye umri wa makamo ameketi hapo, labda mtu aliyepitisha umri ambao angebembana na mwanamke kama huyo, ndipo mwanamke akasema, "Si kawaida, Wewe ukiwa ni Myahudi, kuniomba mimi, mwanamke wa Samaria, kwa fadhila. Hatuna uhusiano." Kwa maneno mengine, "Tuna ubaguzi hapa, na hatuninii. . . hatuna uhusiano."

142 Upesi Yeye akamjulisha. Sasa Yeye alisema, akaongea na huyo mwanamke. Naye mwanamke akasema, "Sasa nyinyi Wayahudi mnasema ni katika Yerusalemu mnaabudu, na, au sisi tunaabudu katika mlima huu," na kadhalika, na jinsi kisima kilivyokuwa kirefu, na Yeye hakuwa na kitu cha kuchotea.

143 Na, mazungumzo, sasa itakubidi kuchukua neno langu hapa kwa hili, kile Yeye alichokuwa anafanya, unaona.

144 Baba, katika Yohana Mtakatifu 5:19, Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda lolote Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda." Sasa kulingana na Neno Lake Mwenyewe. Na Yeye hawezi kusema uongo, na awe ni Mungu. Kulingana na Neno Lake Mwenyewe, Yeye kamwe hakufanya mwujiza mmoja mpaka Mungu alipomwonyesha katika ono, jambo la kufanya. "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda lolote Mwenyewe; ila lile amwonalo Baba analitenda, hilo atenda Mwana pia. Mnaona, Baba afanya kazi, nami nafanya kazi pia."

145 Sasa Baba alikuwa amemwambia Yeye aende huko juu kupitia Samaria, na hapo Yeye alikuwa ameketi hapo, ndipo

basi mwanamke huyu akaja. Sasa ilimbidi Yeye kuwasiliana na roho yake, kwa hiyo ilimbidi Yeye kufanya mazungumzo na huyo mwanamke. Unaona? Na Yeye akasema, baada ya Yeye kupata shida ya mwanamke huyo, sote tunajua ilikuwa ni nini, Yeye alisema, "Nenda kamwite mumeo mje hapa."

146 Naye mwanamke akasema, "Sina mume." Loo, ni kemeo kali jinsi gani Kwake. Unaona? "Nina . . ." Hata hivyo, mwanamke huyo hakujua. Alikuwa tu ni mtu wa kawaida. Hakuvalia kama kuhani yeyote au rabi. Yeye alikuwa tu ni mwanadamu. Unaona?

Kisha kasema, "Nenda kamwite mume wako na mje hapa."

Mwanamke akasema, "Mimi, sina mume."

147 Yeye akasema, "Umesema kweli. Kwa kuwa umekuwa na watano, na yule unayeishi na yeye sasa si wako; katika hilo umesema kweli."

148 Sasa ninawatakeni mtambue tofauti kati ya mwanamke huyo na wale makuhani wenye elimu waliomwita "Beelzebuli." Punde tu alipoona hilo, alisema, "Bwana, natambua kwamba Wewe ni nabii. Sasa, sisi Wasamaria, tunajua Maandiko. Tunajua kwamba ajapo Masihi, aitwaye 'Kristo,' Yeye atafanya hili. Yeye atatwambia mambo haya. Unaona, hiyo ndiyo ishara ya Masihi. Kwa hiyo hapana shaka Wewe ni nabii Wake, kwa sababu Yeye anaenda kuwa nabii wakati Yeye akija. Hatujakuwa na mmoja kwa mamia ya miaka. Lakini wakati Yeye akija, tunajua kwamba Masihi anaenda kufanya hili."

Yesu akasema, "Mimi Ndiye, ninayezungumza na wewe."

149 Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, ni ishara ya Masihi leo, kwa sababu Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Haikuwa ishara kwa wanatheolojia. Ilikuwa ni ishara kwa waaminio.

150 Mwanamke huyo alijua mengi kuhusu Maandiko kuliko hao makuhani walivyojua. Nitasema jambo moja, mwanamke huyo alijua mengi kumhusu Yeye zaidi ya wahubiri wengi wa leo hii. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Naam, mwanamke huyo alimjua Yeye. Kwa nini? Ninaamini kwamba mbegu ya Uzima wa Milele ilikuwa ndani ya mwanamke huyo. Basi wakati hiyo Nuru ilipoangazia Hiyo, upesi aliitambua Hiyo.

151 Sasa watazameni wale makuhani waliopaswa kujua vema zaidi. Walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli. Yeye anafanya hili, Yeye ni . . ."

152 Na Yesu akawaambia, "Kumwita Roho wa Mungu 'roho mwovu,' hakutasamehewa kamwe." Ilikuwa ni Roho wa Mungu akifanya hayo. "Kazi za Mungu, 'roho mchafu.'" Na hao makuhani, badala ya kuchunguza Maandiko! Akasema, "Kama mngaliijua siku Yangu."

153 Kama tungalijua tu ni siku gani tunayoishi, hakungekuwa na mchafuko mwingi hivi kuhusu Ujumbe huu na kuhusu Maandiko

ambayo tunajaribu kuwaletea watu, kama watu wangeelewa tu kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho.

154 Sasa, lakini, wakati Nuru hiyo ilipomwangukia maskini mwanamke huyo, katika hali hiyo, jina baya, mwa—mwa—mwanamke kahaba; na ikiwa Andiko hilo, ikiwa hilo Neno, hilo Neno lililotambulishwa . . . Mwanamke huyo alikuwa amesoma Andiko na alijua kile Neno lilichosema. Basi wakati alipoliona Neno hilo likidhihirishwa, upesi alitambua Hiyo kuwa ni Masihi.

155 Kama aliweza kufanya hivyo chini ya hali hizo, inatupasa kufanya nini usiku wa leo kama tungeweza kumwona Yeye akifanya jambo lile lile, Kanisa lililozaliwa upya na kujazwa na Roho Mtakatifu, linalotazamia Kuja Kwake? Hilo linapaswa kuacha tupu kila kiti cha magurudumu hapa. Jamani, kila mwenye dhambi anapaswa kuanguka karibu na madhabahu. Inathibitisha kwamba Yeye yu hai.

156 Angalia, upesi mwanamke huyo akakimbia kuingia mjini, na kuwaambia watu, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya." Sasa labda mazungumzo yake yalikuwa hivi, "Wanaume na ndugu, hebu niwazungumzie kwa njia huru. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Akasema, "Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?"

157 Ndipo Yesu akaja mjini. Na Biblia ilisema kwamba watu wa mji huo walimwamini Yeye kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyo. Yeye hakufanya Hilo mara nyingine zaidi. Hakusema jambo lingine zaidi kuhusu Hilo. Hilo lilitosha. Yeye alikuwa ndiye Neno la Mungu lililothibitishwa. Alikuwa. Yeye ni Mungu, Masihi. Sasa, kwa taifa la watu namna hiyo! Unaona?

158 Sasa sijui kabisa kwamba ni muda gani zaidi tulio nao. Tutasimama tu labda . . . Vema, ngoja tu kidogo. Yesu alisema, katika Luka Mtakatifu, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Mnakumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa hebu tusimame tu kwa ajili ya Andiko moja zaidi, tuchunguze tu hili kabisa.

159 Sasa, tazama, Yeye alijitambulisha Mwenyewe. Sasa, tunazo sehemu zingine nyingi. Tunaweza kumchukua Bartimayo kipofu, na kotekote, na kuonyesha yule mwanamke akiligusa vazi Lake, mambo yote kupitia Maandiko, na kwenye kisima ambapo Yeye alienda pale, na kujua kwamba mtu yule pale kwenye lango liitwalo Zuri, alikuwa amekuwa na shida hii kwa miaka mingi sana, na kadhalika, na Yesu alijua. Na halafu akaendelea, na kadhalika, kupitia Maandiko, kuendelea kote tangu Mwanzo. Bali, kuwafanya mjue, ili tu kwamba tuweze kuharakisha.

160 Sasa, Yesu alijitambulisha Mwenyewe, thibitisho la Kimaandiko kwa Wayahudi, kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, kwa kuwa nabii. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Huyo alikuwa ni Yesu jana, kwa nabii, ama kwa Wayahudi.

161 Wakati huo Mataifa hawakuwa wakimtazamia Yeye. Tulikuwa makafiri, tukiwa na rungu mgongoni mwetu. Na sisi tukiabudu sanamu, sisi Mataifa. Hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote, kwa hiyo Yeye hakuja kwetu. Injili haikuhubiriwa kwa—kwa—kwa Mataifa mpaka Petro alipowafungulia Injili kwenye nyumba ya Kornelio, muda mrefu baadaye. Ndipo basi Paulo baadaye akasema, "Tazama, ninawageukia Mataifa," baada ya Wayahudi kumkataa.

162 Tazama sasa. Usikose hili. Sasa hili litakusaidia ikiwa tu utasikiliza. Ni kwa nini Yeye hakuifanya ishara hii mbele za Mataifa? Aliifanya mbele za Wa—Wayahudi, Yeye aliifanya mbele za Wasamaria, lakini hakuna wakati mmoja ambapo Yeye aliifanya mbele za Mataifa. Lakini Yeye alibashiri ingefanywa mbele za Mataifa. Kwa kuwa, kile alicho Mungu, Yeye hawezi kubadilika. Kama Yeye alitoa ishara hiyo ili kujitambulisha Mwenyewe miongoni mwa Waebrania na miongoni mwa Wasamaria, kabla tu hawajakatiliwa kutoka kwa Injili, na sisi tumekuwa na miaka elfu mbili ya mafundisho ya Biblia, na sasa Mataifa wamefikia mwisho wao. Ni mwisho kwetu sisi. Ndipo basi kama Yeye akituachilia tuingie juu ya, mafundisho tu ya kawaida ya Presbiteri, Baptisti, Methodisti, ama kadhalika, bila ya kujitambulisha Mwenyewe kikamilifu miongoni mwetu kama Yeye alivyofanya wakati ule, Yeye alifanya jambo lisilofaa. Kwa hiyo Yeye hapendelei mtu, na Yeye alisema Yeye angefanya hivyo.

163 Sasa tazama, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," hapo ni wakati Mataifa walipochomwa, walipoteketezwa. Sasa, Nuhu, Yeye alimtaja Nuhu, hayo yalikuwa ni maadili ya watu, waliingia. Lakini hebu waangalie Mataifa, kabla tu ya moto kushuka kuwaangamiza Mataifa, Wasodoma na Gomora, na miji iliyo karibu nao.

164 Mtazame Ibrahimu, mfano wa Kanisa, huru, Kanisa la kiroho. Lutu, mfano wa kanisa vuguvugu, huko Babeli...au si Babeli; katika Babeli leo hii, bali katika Sodoma wakati ule. Ndipo basi Wasodoma, wasioamini.

165 Daima yapo matabaka matatu ya watu. Tu—tunayo hapa, tunayo kila mahali. Hayo ni waaminio, waaminio wa kujifanya, na wasioamini. Na tunao kila mahali, na matabaka matatu ya watu.

166 Mungu anakamilika katika tatu. Kama vile Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, hufanya Mungu mmoja. Basi kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, hufanya kuzaliwa

kumoja. Maji, Damu, na Roho, hufanya Kuzaliwa kumoja. Na kadhalika, unaona, ni yote, ni kamilifu. Hatuna wakati kupitia ta—tarakimu za Mungu, katika Yake, kile Yeye alichokamilishwa ndani yake; na kile ambacho Kuja Kwake kutakuwa ndani yake, na kadhalika, na ni idadi gani, bali tuko ndani yake.

167 Angalia sasa tunaposoma, tunaona sasa Yule, huyu Masihi. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na kama siku za Lutu." Sasa Ibrahimu alikuwa anamngojea mwana aliyeahidiwa. Ndivyo na sisi. Kanisa lililoitwa litoke, linalowakilisha watu waliozaliwa tena ambao wamejitenga wenyewe na ulimwengu. Hawako Sodoma. Wameitwa wakatoka, wakatengwa, wakishikilia ahadi ya Mwana ajaye.

168 Basi, sasa, siku moja wakati Ibrahimu alipokuwa ameketi katika nchi kame.

169 Na Lutu akiishi na ninii yake mashuhuri. . . hapana shaka yeye alikuwa ndiye meya wa jiji, hakimu. Akawa mtu mashuhuri. Bibi Lutu alikuwa akikata nywele zake na kufanya chochote alichotaka, nadhani, huko chini pamoja na Wasodoma wengine. Bali si Sara; ilinibidi tu kuingiza hilo, ndugu. Tazama, yeye aliishi vyovyote alivyotaka. Alikuwa ni mwanamke maarufu sana. Alichukia kuacha hayo.

170 Bali si Sara. Yeye alikuwa huko juu pamoja na mume wake. Aliitwa akatoka, akatiwa muhuri, kwa ahadi kwamba alikuwa anaenda kuwa na kuzuriwa na Mungu, mwana alikuwa anakuja.

171 Na vivyo hivyo na Kanisa lililowakilishwa na Sara leo hii, limeitwa likatoka, nje ya Sodoma, likiwa na ahadi inayongojea ya Mwana ajaye. Amina. Likiuacha ulimwengu kufanya chochote utakacho kufanya; hiyo haimshughulishi hata kidogo. Yeye ameweka nia yake kwenye ahadi.

172 Kulifanyika nini? Ibrahimu aliinua macho yake akatazama, ndipo akaona watu watatu wakija. Na hivi ulitambua? Ibrahimu, wakati alipowaona watu hao watatu, alisema, "Bwana wangu, hivi Wewe utasimama kwangu?" Kulikuwa na watatu wa hao. Akasema, "Bwana wangu," umoja.

Wakati Lutu alipowaona wawili wao, alisema, "Bwana zangu."

173 Ibrahimu alijua kile alichokuwa anazungumzia. Akasema, "Bwana wangu." Watatu wa hao, na, "Bwana wangu."

Lutu aliona wawili wao, akasema, "Bwana zangu."

174 Kwa hiyo akasema, "Bwana wangu, karibu." Ndipo wakasimama. Mnajua mazungumzo hayo.

175 Angalia sasa, Lutu alikuwa huko chini Sodoma. Basi Malaika wawili wakashuka kwenda Sodoma, kuhubiri Injili, kumwita mwenye haki kutoka miongoni mwa wasioamini. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Billy Graham mamboleo. Hawakutenda miujiza mingi; kuwapiga kwa

upofu, ambako, kuhubiri Neno humpofusha asiyeamini. Bali kikamilifu, Billy Graham mamboleo.

176 Na hivi mliwahi kutambua? Kati ya watu wote mashuhuri tuliowahi kuwa nao ulimwenguni, wahubiri, tangu siku za Yesu Kristo; Sankey, Moody, Finney, Calvin, Knox, kadhalika, kuendelea na kuendelea, na kuendelea na kuendelea, hatujawahi kuwa na mtu huko ambaye jina lake liliishia na h-a-m, kama Abraham, bali G-r-a-h-a-m. Lakini angalia, herufi sita, G-r-a-h-a-m, sita. A-b-r-a-h-a-m ni saba. Hatujawahi kuwa nalo, bali kuna mjumbe huko chini Sodoma, "Tokeni kwake." Naye Mungu amemtuma mtu anayestahili, Billy Graham, akiwaita kutoka Sodoma. Na wao walipokea ishara ya kuhubiriwa kwa Injili. Na wao wanaipata Hiyo leo hii, ulimwenguni kote, kupitia ndugu wa thamani, maarufu, Billy Graham, akiwa na ujumbe wa wokovu, na, "Tokeni Sodoma!" Hiyo ni kweli. Huku jina lake linaishia, *h-a-m*, linamaanisha "baba wa watu, au mataifa."

177 Lakini kulikuwa na Mjumbe, pia, aliyekaa na Abraham, A-b-r-a-h-a-m. Basi tazama, kama Yeye alivyosema, Yeye aliwapa ishara.

178 Sasa kumbukeni, jina lake lilikuwa Abramu, siku chache hapo kabla; Sarai, si Sarah. Jina lake lilikuwa Abramu, sio Abraham. Tazama, Mtu yule aliyeketi na kuzungumza na yeye, kasema, "Ibrahimu, yu wapi Sarah, mkeo?"

179 Sasa wanawake katika siku hizo si kama walivyo leo hii, inawabidi kukimbia nje na kuingia katika shughuli ya mume, na kuendesha shughuli hiyo na kila . . . Unaona, walikaa nyuma palipo mahali pao. Lakini, wao, alikaa ndani ya hema.

Ndipo Yeye akasema, "Yuko wapi Sara mkeo?"

180 Sasa angalia kile Biblia ilichosema. Ibrahimu alisema, "Yuko ndani ya hema, nyuma Yako." Malaika alikuwa amegeuza mgongo Wake kuelekea hema.

181 Naye Malaika huyo alikuwa ni Mtu, kwa sababu Yeye alikula nyama ya ndama, akanywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na kula ugali na siagi. Hiyo ni kweli. Alikula. Alikula na kunywa pamoja na Ibrahimu, huku alichukua tawi la kufukuzia nzi na kuwafukuza nzi kutoka Kwake, huku Yeye akisimama pale na kunywa. Hiyo ni kweli, Mwanadamu!

182 Ndipo Yeye akasema, "Ibrahimu, mimi . . ." Na hicho ni kiwakilishi nafsi, tena. "Nitakuzuru kulingana na ahadi." Huyo alikuwa ni Nani?

183 Na Sara, akisikiliza, akitega sikio kisiri, mwajua, alicheka kifichifichi, kwa namna fulani, moyoni. [Ndugu Branham anaigiza—Mh.] "Mimi, mwanamke mkongwe, umri wa miaka mia moja, uhusiano wa kifamilia ulikuwa umekoma kwa miaka mingi; mimi nipate raha na bwana wangu tena, nikiona kuwa yeye ni mkongwe?"

184 Ndipo Malaika, huku ameelekeza mgongo Wake kuelekea hema, kasema, “Ni kwa nini Sara akacheka?” Amina!

185 Tazama wakati Malaika alipotoweka na kuondoka, Ibrahimu alimwita, “Elohimu.” Msomi yeyote anajua kwamba popote uonapo herufi kubwa B-w-a-n-a, inatafsiriwa katika Kiyunani, *Elohimu,* “Yule ajitoshelezaye kwa yote, Yule mwenye nguvu,” Ambaye ni Yehova Mungu. Utukufu!

186 Mtu aliniambia, “Unataka kuniambia, wewe unaamini kwamba huyo alikuwa ni Mungu?”

187 Nikasema, “Ibrahimu aliongea na Yeye, na yeye akamwita ‘Mungu.’ Anapaswa kujua.” Loo, nina furaha sana kwamba ninamjua Mungu namna hiyo!

188 Yeye alifanya nini? Kile ambacho ninafikiri Yeye alifanya kilikuwa. . . Unajua, sisi tumeumbwa kutokana na elementi kumi na sita mbalimbali za udongo, mwajua: petroli, na nurulimwengu, na potashi, na kalishi. Ninaamini Yeye alisema tu, “Nimesikia kuhusu hizo dhambi. Nitakuja, niende huko chini na nione hiyo. Njoo hapa, Gabrieli,” akakusanya konzi moja la nurulimwengu, na, Phfff! “Ingia katika huo. Na njoo hapa, Woodworm,” na, Phfff! “Ingia katika huo.” Ndipo akajitwalia Mwenyewe moja. Kwa nini? Yeye ni Mungu.

189 Nina furaha sana kujua. Kwamba, siku moja huenda nisiwe chochote ila nirudi kwenye nurulimwengu. Huenda nisiwe chochote ndani yake uwezacho kupata. Mifupa hii huenda ikaozea mbali, lakini Yeye anajua jina langu. Siku moja Yeye ataniita; nitatokea katika sura Yake.

Huyo ni Mungu wetu. Ibrahimu alimwita “Elohimu.”

190 Tazama, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Wajumbe watakuwa Sodoma; na Kanisa lililoitwa litoke litapokea ishara, ya kitu gani? Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa mwanadamu. Utukufu! Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni ishara kwa Kanisa la Mataifa. Sasa ni wakati wetu. Ni sisi kuona hiyo, ahadi ya Mungu. Tungeweza kusimama hapa kwa saa moja, huku na huku, kupitia Maandiko, na kusokota hiyo pamoja na kuthibitisha kwamba hiyo ni sahihi. Na hii ndiyo saa. Hii hapa ishara ya mwisho kuonekana. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

191 Kitabu cha Ufunuo, katika Nyakati za Kanisa, Wakati wa Kanisa la Laodikia, malaika wa saba alipaswa. . . Katika siku za sauti ya huyo, “siri ya Mungu inapaswa kukamilika.” Na sisi tuko katika Wakati wa Laodikia; wazembe, wanyonge, wasiofaa kitu, vuguvugu, na hiyo ndiyo hali kanisa letu la Pentekoste limeingia ndani yake. Mungu ametikisa kila karama ambayo Yeye aliweza mbele zetu.

192 Inanikumbusha, kama maskini mama mmoja huko Louisville, hapa si muda mrefu uliopita. Alikuwa na mvulana mdogo, akitembea kote, akijaribu kutikisa wanasesere wadogo, naye mtoto huyo aliketi tu na kukodoa macho. Na watu walimwangalia. Ndipo akaanza kupiga mayowe. Alipanda juu, baadhi ya wanawake, na wakamwuliza kuwa shida ni nini. Kasema, "Mvulana wangu mdogo amepatwa na mpagao juu yake." Na kasema, "Yeye hatatambua vitu kama watoto wanavyopaswa kutambua, umri wake." Tena kasema, "Nilimpeleka kwa daktari, naye daktari akasema alikuwa afadhali, bali," kasema, "hayuko afadhali." Kasema, "Ninatikisa maskini mwanasesere huyu, maskini mtoto yeyote. . . Na yeye anaketi tu na kukodoa macho. Mtoto yeyote anafaa kutambua huyo kuwa ni mwanasesere, na kumfikia, lakini yeye anakodoa tu macho."

193 Hicho ni kitu kama kanisa la Pentekoste. Mungu amemtuma Oral Roberts, na kila kitu kingine, kote, wakitikisa kila namna ya karama na kadhalika, kwa kanisa. Yeye amemwaga Roho Wake. Mmenena katika lugha, mkatafsiri, mkawa na karama za unabii, na kila kitu kingine.

194 Na umefikia wakati kwa Yesu Kristo kujitambulisha Mwenyewe miongoni mwa watu, yeye yule jana, leo, na hata milele, ambayo itakuwa ndiyo ishara ya mwisho itakayotikiswa mbele za watu. Kumbukeni, kitambo kidogo baada ya madhihirisho hayo ya Mungu katika umbo la binadamu, katika mwili, moto ulishuka na kuwameza Mataifa. "Na kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu."

195 Yeye alijitambulisha Mwenyewe kama Masihi, kwa Wayahudi, kwa kutambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwao, kwa kuwaambia majina yao na mambo mbalimbali. Walijua huyo alikuwa ni nabii ambaye Bwana Mungu aliahidi kumwinua. Hao wa halisi, wa kweli waliokusudiwa kimbele kwa hilo, waliliona.

196 Kama hakuna kitu moyoni kupokea hilo, basi hakuna kitu mle. Unawezaje kupata damu kutoka kwa tanipu? Hamna damu ndani yake. Basi mtu anawezaje kuamini kama hakuna kitu humo ndani cha kuamini nacho?

197 Lakini ikiwa Roho Mtakatifu yumo humo ndani, upesi hulishika hilo Neno. Huyo huruka upesi, unaona, hushika Hilo haraka. Sasa, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Yeye aliahidi hapa kujitambulisha Mwenyewe miongoni mwetu, sawa na jinsi Yeye alivyofanya.

Sasa unasema, "Lakini Yeye angewezaje kujitambulisha Mwenyewe?"

198 "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena. Hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja

nanyi, hata ndani yenu." Ni Roho Mtakatifu ndiye anenaye kupitia lugha na kutoa tafsiri, Yeye yule ambaye hukuokoa kutokana na dhambi. Ni Yesu Kristo yeye yule, amekuja.

199 [Dada mmoja ananena katika lugha nyingine. Mtu mwingine anaanza kunena katika lugha nyingine, halafu sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Tatu. [Sehemu nyingine tupu kwenye kanda.] Sifa kwa Bwana. Mlitambua hilo? Inaendelea kusema, "Tokeni, tokeni, tokeni," unaona, kuitwa utoke. Vema, mnasikia kile hicho kilicho.

200 Sasa Biblia inanena, iwapo kuna wageni hapa, Biblia inazungumza kuhusu kunena katika lugha na tafsiri, unaona. Kwa hiyo basi ikinenwa katika lugha na kutafsiriwa, basi ni unabii. Unaona, hiyo ni kweli, sivyo? Ni unabii.

201 Sasa tokeni. Sasa Bwana anaonekana kuwa anasema Yeye anaenda kukupa nafasi sasa, unaona, kitu ambacho hujawahi kuona hapo kabla, kitu ambacho Yeye anaenda kufanya. Sasa hebu tuamini hilo kwa moyo wetu wote.

202 Sasa tunaninii tu, mimi na Billy, tulipoenda India safari hii ya mwisho, sisi. . . nina kijipande kutoka kwenye karatasi. Nayo ikasema, "Te—tetemeko la ardhi hapana shaka limeisha." Siku chache kabla hatujafika huko, walijua. . . Unaona, India haina nyua kama mlizo nazo hapa, nyua za waya. Wanaokota mawe, nao wanatengeneza majengo yao mengi. Wao ni watu maskini kwelikweli. Na—na maskini ndege hujenga viota vyao kwenye miamba hii, na halafu ng'ombe na kondoo wanaingia, jioni, na kusimama kuzunguka kuta hizi, wakati jua linawaka, kupata baridi.

203 Lakini walitambua, kwa siku kadhaa, ng'ombe hawakuingia, walibaki moja kwa moja huko uwanjani. Kondoo walikusanyika pamoja na kubanana mmoja na mwenzake, na kuegemeana, uwanjani, kupata baridi. Ndege wote waliruka wakatoka kwenye kuta. Hawakujua kilichokuwa kinaenda kufanyika. Ndipo tetemeko la ardhi likapiga, na kuporomosha hizo kuta. Ndipo maskini ndege wakarudi na kujenga viota vyao tena katika malundo ya miamba, na ng'ombe wakaanza kuingia tena.

204 Sasa, tazama, kama huyo siye Mungu yule yule aliyeweza kuwaonya waingie ndani ya safina, katika siku za Nuhu! Na ikiwa Mungu angeweza kufanya hilo, na kuwaonya ndege, kwa silika; na kuwaonya ng'ombe na kondoo, kwa silika, kuondoka kwenye kuta hizo kubwa za kale zinazoenda kuanguka. Mungu anajaribu kuwaonya watu Wake leo hii, kuondoka kwenye kuta hizi za kale za kikanisa ambazo zinaenda kuporomoka, moja ya siku hizi, kwa kuwa Kuja kwa Bwana kumekaribia.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

205 Bwana Yesu, ninajihisi kwamba ni wakati wangu kusimama sasa. Na ni wakati Wako kunena, Baba. Nimejaribu kuwaambia

watu kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nimejaribu kuthibitisha hilo kwa Maandiko, kile Wewe ulichokuwa, na jinsi ambavyo Wewe ulijitambulisha Mwenyewe.

206 Basi ninakumbuka tena, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 14 na kifungu cha 12, Wewe ulisema, "Yeye aaminiye," si anayejifanya kuamini, "yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo atazifanya pia." Ingewezaje kufanya jambo jingine tofauti, Baba? Kama tungeweza kuhamisha uhai kutoka kwa mpea hadi kwa mpichi, ungezaa pea, kwa kuwa uhai wa mpea uko ndani ya mpichi. Pia, Baba wa Mbinguni, kama Uhai uliokuwa ndani ya Kristo, nia iliyokuwa ndani Yake, Roho aliyekuwa ndani Yake, ameahidi kuwa ndani yetu, basi tunashuhudia huyo. Kama Yeye ndiye Mzabibu na sisi ni matawi, Uhai hutoka kwenye Mzabibu. Bwana, jalia tuwe matawi, usiku wa leo. Tunatambua kwamba mzabibu hauzai tunda lolote; ulitoweka, bali ulirudi katika hali ya Uhai, nayo matawi huzaa tunda. Sauti yako ni wakati Wewe unaponena kupitia sisi. "Ukiuambia mlima huu ng'oka, na usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba kile ulichosema kitakuja kutimia, unaweza kupata ulichosema. Unapoomba, amini unapokea kile ulichoomba, utapewa." Ee Mungu, ahadi kama hizo! "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, basi ombeni mtakalo."

207 Ee Mungu, ahadi kwelikweli kanisa lililo nazo, na ukombozi mkamilifu kwelikweli! Tunatambua kwamba sisi hatustahili, na kamwe hatutastahili. Hakuna njia kwetu kustahili. Na hatuhesabu kustahili kwetu. Tunatazamia Dhabihu yetu, Bwana Yesu. Yeye ndiye Yule tuliyefichwa ndani yake, usiku wa leo. Tumehifadhiwa katika ahadi Yake iliyobarikiwa, katika Neno Lake. Hilo ni ninii letu . . .

208 Hapo ndipo mahali pa kujificha kwa imani, juu ya Mwamba usiotikisika wa Neno la Mungu la Milele. Imani huchukua mahali pa—pake panapostahili hapo, mahali pake, hakuna kitu kiwezacho kuitikisa. Mauti hayawezi kuitikisa na kuiondoa. Kaburi haliwezi kuificha. Imethibitishwa. Katika siku ya tatu Yeye alifufuka, kwa sababu Neno la Mungu lilisema, "Sitaiacha nafsi Yake kuzimuni, wala sitamwacha mtakatifu Wangu aone uharibifu." Hakuna kaburi lingaliweza kumshika Yeye.

209 Ee Mungu, ni Neno Lako. Lifanye lidhihirike usiku wa leo. Wewe ni Neno. Pia jalia Maneno uliyoahidi, yanenwe usiku wa leo, Bwana, tena jalia ishara kwamba Masihi yuko duniani, na sisi tuko wakati wa mwisho. Kama mamajusi walivyoona nyota tatu zikipangana, kuwa moja; na kama tunavyoona, leo hii, Bwana, sifa tatu za Mungu hatimaye zimeingia katika mkondo, tunajua hizo ni moja. Na tunaona ishara hizi zote kuu juu ya nchi, zinazoonekana; na utambulisho wa Mwana wa Mungu, akifanya kazi katika mwili wa Kanisa Lake, kuendeleza kazi Yake. Mungu, naomba mioyo ya wanadamu itetemeke. Jalia wenye dhambi watikisike. Pia jalia kuwe na toba, na ninaomba

kuwe na uponyaji kwelikweli, usiku wa leo, wa nafsi na mwili pia, ili wanaume na wanawake, kila mahali, wataondoka kwenye kutokuamini, wajitenge wenyewe na kumwamini Mungu aliye hai.

210 Ninajikabidhi mwenyewe Kwako, Bwana, kama mtumishi Wako. Ninakabidhi kanisa hili Kwako. Ninatambua, Bwana, haijalishi ni kiasi gani Wewe ungenitia upako, ikiwa watu hawauamini, basi haiwezi kufanywa. Sote wawili hatuna budi kufanya kazi kama mwili mmoja wa imani ya Mungu, na ya heshima ya Neno la Yesu Kristo, kuona mambo haya yakitendeka.

211 Tunaulizwa swali, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Pia, Baba, Wewe umeahidi hilo, kwamba Wewe ungekuwa pamoja nasi. Sasa tutakutazamia Wewe kuonekana miongoni mwetu, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo ninaomba mambo haya. Amina.

212 Sasa ninaamini . . . na kama kadi za maombi zilisambazwa. Moja hadi mia moja? Vema, hebu sisi, hatuwezi kuwasimamisha wote kwa wakati mmoja, inatubidi tu kuwaleta mmoja mmoja. Sasa wakati . . . Tutawaita, mmoja mmoja, na halafu ikiwa wewe ni kiwete, umepooza, huwezi kusimama, baadhi ya ndugu hawa watakuja, wakulete kwenye jukwaa, ili kuombewa.

213 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . simama. Kama huwezi, unijulishe. Namba mbili, kadi ya maombi namba mbili, naomba usimame. Asante.

214 Namba tatu, ni nani aliye na kadi ya maombi namba tatu? Waweza kusimama? Upesi sana sasa, hatuna budi kuharakisha. Je! ni mama huyu, aliye na namba tatu, kadi ya maombi? Vema. Vema, shuka chini uende mwisho pale, namba tatu. Billy, wewe au mtu mwingine aje hapa.

215 Namba nne, namba nne, kadi ya maombi namba nne, ni nani aliye nayo? Huko nyuma kabisa. Vema, njoo hapa, mama. Namba tano. Nyote mtaitwa, mmoja mmoja. Namba tano.

216 Unayo kadi gani, bwana? [Ndugu huyo anasema, "Namba tatu, B."—Mh.] Namba gani? ["Tatu."] Namba tatu? Mtu fulani amekosea. Mwa—mwanaume huyu hapa anayo kadi namba tatu. Vema.

217 Namba nne, ni nani aliye na namba nne, kadi ya maombi namba nne? Vema, namba tano, ni nani aliye na kadi ya maombi namba tano? Namba sita, ni nani aliye na hiyo, namba sita? Asante. Njoo. Namba saba. Sasa chukueni tu mahali penu. Namba saba. Namba nane, nane.

218 Tisa, tisa, hivi niliiona? Tisa, mtu fulani aharakishe sasa kusudi tusichukue muda mwingi sana kwao. Namba tisa, kadi ya maombi namba tisa, tafadhali. Mtu fulani anisaidie kuangalia. Nyinyi ndugu simameni na mnisaidie kuangalia. Namba tisa,

haipo hapa? Vema, ikiingia, inaweza kuchukua mahali pake; huenda ametoka nje, nilihubiri muda mrefu.

219 Namba kumi, kadi ya maombi kumi, inua mkono wako juu ili tuweze kuona wewe ni nani. Vema, njoo. Kumi na moja, kadi ya maombi kumi na moja. Hivi hukuwa nayo, mama? Inueni mikono yenu nikiwaambia, halafu wewe, wakati namba yako ikiitwa, basi wewe—wewe utajua.

220 Namba kumi na mbili, namba kumi na mbili, ni nani aliye nayo? Namba kumi na mbili. Njoo, mama. Namba kumi na tatu, kadi ya maombi kumi na tatu. Huko nyuma kabisa. Njoo, mama, kama unaweza kusimama. Namba kumi na tatu. Namba kumi na nne, namba kumi na nne, iko wapi? Kadi ya maombi kumi na nne, huko nyuma kabisa. Vema, njoo moja kwa moja mbele, mama. Namba kumi na tano, mwanaume huyu papa hapa, namba kumi na tano. Kumi na sita, kumi na sita, kumi na sita, kadi ya maombi namba sita-. . .Huko katika kona. Kumi na saba.

221 Unaona, si uwanja wa michezo, hatuninii . . .Tu—tunawaita, mmoja mmoja; hamna mbio kubwa huku na kuruka ndani, mwajua. Tunataka utaratibu, unaona, uchaji.

222 Namba kumi na sita, kadi ya maombi namba kumi na sita. Namba kumi na sita, je! huyu mama anayo kumi na sita? [Mtu fulani anasema, "Kumi na nne."—Mh.] Kumi na nne. Namba kumi na sita, kumi na sita. Vema, asante, bwana. Namba kumi na saba. Tayari yuko chini, naam, kumi na saba. Kumi na nane. Vema. Naam.

223 Vema, tayari wameleta wengi sana huko juu wawezao kusimama kwenye kona wakati huu. Tutaanza, moja kwa moja katika dakika chache, kuanzia hapo. Vema.

224 Ni wangapi wenu, wakati wakiwapanga hao watu mstarini, ambao hamna kadi ya maombi, hebu tuone mikono yenu, nanyi ni wagonjwa? Vema, huku nikiwanukulia Maandiko. Sasa wewe huna kadi ya maombi, hata hivyo wewe ni mgonjwa, hutaitwa kwenye mstari wa maombi? Vema.

225 Ni wangapi katika jengo hili ambao hawanijui, na wanajua sijui chochote kuwahusu, inueni mikono yenu; ambao ni wagonjwa, mnajua. Unaona? Kusema kweli, sioni mtu mmoja ninayemjua. Sasa, huenda ukanijua, bali kwa kweli . . .Si—simaanishi hili kupitia madhara yoyote, sijawahi kuwaona, na si—si—sioni, siwezi kuona mtu mmoja ambaye ni—ninamjua, isipokuwa ni maskini jamaa huyu ambaye kidogo ni mnene anayeketi hapo, maskini . . .Je! ninamwangalia mtu sahihi? Ninasahau jina lako, unatoka Missouri. Ni—ninajua yeye huja maskanini mara moja moja.

226 Sasa, na kwenye jukwaa, sasa, kumbukeni, Mungu yuko tu kiasi kile jukwaani kama Yeye alivyo huko nje. Simjui yeyote hapa, kusema tu kwamba ninawajua, mbali na ndugu huyu papa

hapa, na Ndugu Moore, kujua kweli jina au kumjua yeyote. Huenda nikajua. . . Na—nafikiri huyu ni baba yako aliyeketi hapo nyuma, nina hakika kabisa hiyo ni kweli. Na Jim Maguire hapa, m—mvulana wa kanda anayeketi hapa. Na hao ndio wote ninaowaona, kujua, na kujua kuwa wao ni kina nani. Vema.

227 Sikilizeni, hebu tuchukue tu hadithi fupi namna hii wakati wanapojiweka tayari, hadithi nyingine ambayo tungeweza kuchukua kumhusu Bwana Yesu. Hapa, ni wangapi wanajua kwamba Biblia inasema kwamba wakati mmoja kulikuwa na mwanamke aliyekuwa anatokwa damu? Naye mwanamke huyo asingeweza, hakuitwa katika mstari wa maombi, pia. Bali, na yeye hakuwa na kadi ya maombi, bali alikuwa na imani, na hiyo ndiyo humgusa Mungu. Na Yesu akitembea barabarani, maskini mwanamke huyu alijipenyeza ndani na kugusa upindo wa vazi Lake.

228 Ni wangapi wanajua kwamba vazi la Kipalestina lilipwaya? Lilikuwa ni joho. Na lilikuwa na vazi la ndani, pia, unaona, kuzuia vumbi isifikie viungo vyao. Kwa hiyo walikuwa na—walikuwa na vazi la ndani, vazi lilizoa vumbi wanapotembea. Basi kwa hiyo walikuwa na vazi la ndani.

229 Ndipo mwanamke huyu aligusa upindo wa vazi Lake, kwa kidole chake. Na Yesu akasimama, ndipo Yeye akasema, "Ni nani aliyenigusa Mimi?" Siamini Yeye alikuwa tu anafanya mchezo. Siamini Yeye alifanya hivyo. Ninaamini kwa kweli Yeye hakujua ni nani alifanya hivyo. Akasema, "Ni nani aliyenigusa Mimi?"

230 Na jinsi ambavyo, watu wengi walikuwa wamemkumbatia Yeye kwa mikono yao, "Jambo, Rabi! Huyu ndiye Nabii wa Galilaya? Vema, tuna furaha kukuona Wewe hapa." Kila mtu, "U hali gani?"

231 Petro akasema, "Bwana!" Alimkemea, Biblia ilisema. Kwa maneno mengine, Petro huenda alisema hivi, "Mbona, hilo kwa namna fulani linasikika lisilo la kawaida, kwa Mtu wa kiwango Chako kusema 'ni nani aliyekugusa' Wewe. Na ninadhani, tangu nimekuwa nikiongea na Wewe, kumekuwa na mikono hamsini imekugusa Wewe. Na halafu Wewe unasema, 'Ni nani aliyenigusa Mimi?' Mbona, halisikiki sahihi kiakili, Bwana. Hupaswi kusema jambo kama hilo." Biblia ilisema, "Petro alimkemea."

232 Bali Yesu alisema, "Naona kuwa nguvu zimenitoka Mimi." Ulikuwa ni mguso wa aina tofauti, mguso wa imani. Nguvu ni uweza. "Naona kwamba nguvu Zangu. . . Nimekuwa mnyonge. Mtu fulani amenigusa Mimi kwa m—mguso wa imani."

233 Sasa Yeye asingeweza kuuhisi huo, kimwili. Huenda ukagusa koti langu, na yapo mengi zaidi kati ya upindo wa vazi Lake na mwili Wake, kuliko yaliyoko kwa koti langu.

234 Kama tu vile Bartimayo kipofu, akisimama yadi mia moja kutoka Kwake, kasema, "Yesu, Wewe Mwana wa Daudi."

235 Nao watu wote walikuwa wanapiga mayowe, "Tunasikia Wewe uliwafufua wafu. Tunayo makaburi yaliyojaa hao hapa juu. Njoo hapa juu ukawafufue, tutakuamini Wewe." Unaona, hao wapinzani, unaona, na kadhalika.

Bali Yesu hata hakumsikia Bartimayo, ila imani yake ilimsimamisha Yeye. Unaona, imani yake ilifanya hivyo.

236 Sasa, imani ya mwanamke huyu ilimsimamisha Yeye, ndipo Yeye akaangalia kote katika kusanyiko mpaka Yeye akampata maskini mwanamke huyo. Ndipo Yeye akamwambia mwanamke huyo kuhusu hali yake, na kusema, "Imani yako imekuokoa." Je! hiyo ni kweli? Maskini mwanamke tu wa kawaida, anayeonekana mnyonge, na yeye aliponywa.

237 Sasa mwanamke huyo alifanya nini? Kamwe hakumgusa Yeye, hasa. Alimgusa Mungu, kupitia Yeye. Vema, basi hilo... Ni wangapi wanajua...Wahudumu hawa, ambao, ninajua wanajua. Bali Kitabu cha Waebrania kinasema kwamba, "Yesu Kristo sasa ndiye Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Je! hiyo ni kweli? [Wahudumu wanasema, "Amina."—Mh.]

238 Ni wangapi wanajua hilo katika wasikilizaji? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, kama Yeye ndiye Kuhani Mkuu, Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule ambaye Yeye aliwahi kuwa. "Hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na wanadamu, ila Mwanadamu Kristo Yesu." Basi ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na wewe ulimgusa Yeye jinsi yule mwanamke alivyofanya, na Yeye anaweza kuguswa, na kama ungeweza kumgusa Yeye kama Yeye alivyofanya, si Yeye angeitikia kwa njia ile ile ambayo Yeye aliitikia wakati ule, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Je! hiyo ni kweli? ["Amina."] Unaona? Jambo la pekee likupasalo kufanya ni kumgusa Yeye.

239 Sasa, si kumgusa mmoja wa ndugu zetu, au kunigusa mimi. Hao, hao ni ndugu zako tu, unaona. Lakini mguse Yeye. Imani yako imguse Yeye, ndipo Yeye atatumia chombo Chake na Yeye atakuwa...Atafanya vile vile leo hii kama Yeye alivyowahi kufanya. Yeye ni yule yule leo, na milele. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

240 Kwa hiyo sasa ninawatakeni nyote, usikivu wenu mkamilifu, kila mtu kaa moja kwa moja mahali pako kwa dakika chache zijazo, na uombe.

241 Sasa, ni jambo kuu kuja hapa na kuhubiri Injili inayoweza kuwafanya watu, hasa, ambao wakati mmoja walikuwa wauza pombe haramu na wacheza kamari, na makahaba na kila kitu kingine, huko nje mtaani, kuketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, na wanaweza kuhisi uvuvio wa Roho kukuinua kufikia mahali hata unapoteza utu wako mwenyewe, na kupaza sauti "amina" na "haleluya," sifa kwa Mungu. Hilo ni jambo la ajabu. Lakini basi katika wasikilizaji hao hao,

na Injili ikihubiriwa na kusema kile Yeye alichokuwa, sasa kumtambulisha Yeye tena moja kwa moja Yeye yule.

242 Sasa katika mstari huu wa maombi unaosimama hapa, sidhanii. . . Simwoni mtu katika mstari huo ninayemjua. Hakuna mtu. Ikiwa kila mmoja wenu mlio katika mstari huo wa maombi, ni wageni kwangu, sikujui, unajua kwamba sijui chochote kukuhusu, inua mkono wako. Kila mmoja wenu katika mstari wa maombi, anayejua kuwa sijui chochote kukuhusu, inua mkono wako. Vema. Nadhani, ulikuwa ni mstari wote wa maombi. Sasa, simjui hata mmoja wao. Sasa njia ya pekee ambayo. . .

243 Basi ikiwa mtu yeyote anafikiria kuwa huu ni uwongo, wewe njoo hapa juu na uchukue mahali pangu. Unaona? Mpaka unapoweza kufanya jambo lile lile, basi usiseme lolote juu ya hili. Yesu alisema, "Kama ninatoa pepo kwa kidole cha Mungu, watoto wenu wanawatoa kwa nani?" Kwa maneno mengine, "Ni mfumo gani bora walio nao?" Unaona?

244 Sasa tumekuwa na wakati ambapo kila mtu ameanza kuwazia kuhusu desturi ya kale, kuwekea mikono. Na hiyo ni sawa. Lakini sasa, ndugu zangu wahudumu, nishuhudieni tu, hiyo ilikuwa ni desturi ya Kiyahudi. Unaona?

245 Yairo alisema, "Njoo uweke mkono Wako juu ya binti yangu, naye ataishi." Lakini yule Mrumi, Mtaifa, alisema, "Sistahili hata Wewe uje chini ya paa langu. Nena tu neno." Je! hiyo ni kweli? Ni neno likinenwa; Mataifa, unaona. Tunapaswa kuendeleza hilo; kama yule Mrumi angeweza kuwazia hilo, kafiri ambaye ndio kwanza amwone Yeye. Maana, alijua kwamba, Maneno ya Yesu Kristo. Akasema, "Mimi ni mtu chini ya mamlaka. Ninamwambia mtu *huyu*, 'nenda,' naye anaenda, na *huyu* anakuja. Inambidi kufanya hivyo, maana yuko chini yangu." Alikuwa anatambulisha kitu gani? Kwamba kila maradhi na kila ugonjwa ulikuwa chini ya amri ya Yesu Kristo. Naam, bwana. Yeye ana mamlaka.

246 Na iwapo tunaweza kumsikia Yeye akinena, basi hilo humtambulisha Yeye kuwa pamoja nasi. Jinsi ingekuwa kuu zaidi kwenu Mataifa, usiku wa leo, kujua, na kujua kwamba Yeye yuko miongoni mwetu, na tunaweza kuinuka na kutambua. Si kusema, "Ndugu Branham aliweka mikono juu yangu; Ndugu Roberts, ama nanii wangu. . . mtu mwingine." Bali kwa imani katika Mwana wa Mungu, useme, "Ninakukubali Wewe, Bwana Yesu. Wewe upo hapa. Wewe niponye."

247 Sasa kama Yeye atajitambulisha Mwenyewe na kuthibitisha kwa Injili kwamba Yeye yupo hapa sasa kadiri kama Yeye alivyokuwa wakati ule. Nimewathibitishieni, hiyo ndiyo alama Yake ya utambulisho, (hiyo ni kweli?) akiahidi katika siku za mwisho mambo haya yatatendeka. Nasi tumeliona kanisa likiingia moja kwa moja kupitia Luther, Wesley, Pentekoste,

na moja kwa moja kufikia mwisho. Unaona? Na sisi tupo hapa, Wakati wa Laodikia, Wakati wa Sodoma, na sisi tupo hapa. Huduma imekuja kupitia kila pembe ya Neno. Nami ninaamini, siri yote ya Mungu, Hiyo tayari imehubiriwa. Sasa ni utambulisho wa Kristo miongoni mwa watu Wake, Mungu akifanya kazi katika mwili wa binadamu.

248 Sasa, haijalishi ni kiasi gani angeitia yangu upako, huna budi kutiwa upako, pia, kuliamini. Unaona, wewe ndiwe inakubidi kugusa. Unaona? Na sote wawili, pamoja, tunakuwa kitu kimoja. Sikujui wewe; wewe hunijui mimi. Wewe amini tu, na mimi niamini, ndipo Mungu anatuchukua sote wawili mkononi. Huyo ni Mungu.

249 Ndipo, unaona, Biblia ilisema, "Kama nyinyi nyote mkinena kwa lugha, na kuje mmoja miongoni mwenu, asiyeelimika, kuwe hakuna mtafsiri, basi angesema 'Nyinyi ni wendawazimu.' Lakini hebu mmoja atabiri na kufunua siri ya moyoni, basi wote wataanguka chini na kusema, 'Mungu yu pamoja nanyi.'" Nina shukrani kuona siku hiyo ikiwadia, kuishi muda mrefu vya kutosha kuiona miongoni mwa kanisa lililoitwa litoke.

250 Nyinyi kumbukeni, haiendi Babeli. Haikuenda Sodoma. Iliwaendea walioitwa watoke, Wateule; hiyo ndiyo ishara wanayoona. Wana yao huko nje, makundi yao ya kimadhehebu na kufanya yasiyofaa.

251 Bali huyu ni Bwana Yesu Kristo katika umbo la Roho Mtakatifu, akitembea miongoni mwa watu Wake, akifanya jambo lile lile ambalo Yeye alifanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, akijitambulisha Mwenyewe pamoja na Bibi-arusi Wake, si kanisa.

252 Kuna tofauti kati ya kanisa na Bibi-arusi. Sio kuhubiri fundisho, maana sifanyi hivyo; ila, kwa imani yangu nyenyekevu, Bibi-arusi hupitia ninii...ama, ka—kanisa hupitia dhiki kuu, muhuri wa sita, kulitakasa. Hiyo ni kweli. Bali Bibi-arusi hapitii; yeye anaenda katika Unyakuo kabla ya hapo. Ni wakati wa Bibi-arusi kuitwa atoke, kwa hiyo sasa ninaamini ni wakati wa kuitwa kutoka.

253 Samahani, ndugu, sipaswi kuhubiri fundisho, huenda wakawa na...?...Huenda wakatofautiana; ukitofautiana, kama tu kula sambusa ya cheri, tupilia mbali mbegu na ule sambusa. Unaona, hiyo ni kweli. Vema.

254 Bali ninaamini hapo ndipo tunapokosea, ambapo baadhi yetu wanaamini, mmoja, anasema Hilo hupitia. Na huyo mwingine anasema, hakika, kanisa litapitia hiyo; lakini, hakika, lipo kanisa huko Babeli, huko nje Sodoma. Bibi-arusi ameitwa atoke, ameketi hapa juu akimngojea Mwana ajaye. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Hapo ndipo ishara inafanywa, si huko chini miongoni mwa ma—madhehebu; katika wateule.

255 Sasa, mbele za Mungu, Ambaye ninasimama, wala sisemi uwongo, Yeye akiwa ni Hakimu wangu, kwa uchaji ninasema kwamba hakuna mtu kwenye mstari huo, ninayekumbuka kuwahi kumwona maishani mwangu. Hakuna mtu, mbali na hao niliowataja hapa, ambaye ninajua jambo moja kumhusu, au niliyewahi kumwona; nikiwa na Biblia hii hapa mbele zangu.

256 Sasa, kama Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kama nilivyowaambia! Na nyinyi mnajua kwamba mimi si mwanatheolojia, mimi si mhubiri, kama kile ninachokiita kama wachungaji wenu hapa waliopakwa mafuta kuhubiri hii. Huo ni mwito wao. Huu ni mwito wangu, sasa nimetiwa upako na Roho Mtakatifu, kumfanya Mungu atembee kupitia watu Wake. Unaona?

257 Sasa je! mtaamini hilo? Kama Yeye atajionyesha Mwenyewe miongoni mwa watu Wake usiku wa leo, ambao Yeye aliahidi, "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena. Wasioamini hawataniona Mimi. La, wako huko nje katika Sodoma. Bali nyinyi mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Kazi nizifanyazo mtazifanya pia. Nyingi zaidi ya hizi mtafanya."

258 Ninajua King James inasema, "nyingi zaidi," bali wewe chukua Emphatic Diaglott na uone kama haisemi—haisemi . . . King James inasema, "kubwa zaidi." Usingeweza kufanya yoyote kubwa zaidi. Hakuna chochote kinachoweza kufanywa kikubwa zaidi. Yeye aliwaponya wagonjwa, akawafufua wafu, akasimamisha maumbile, akafanya kila kitu kilichokuwepo. "Bali *nyingi* zaidi mtafanya."

259 Kwa sababu, Yeye aliwakilishwa tu ndani ya mtu mmoja pale, Yesu Kristo, Mungu. Lakini sasa Mungu yuko miongoni mwa Kanisa Lake, kila mahali. "Nyingi kuliko hizi mtafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba; kurudi katika umbo la Roho, Baba Roho." Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza watoto kupitia nyikani, iliyokaa ndani ya Yesu Kristo, ilirudi kwa Mungu, na ikasema, "Nalitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu."

260 Angalia kilichotendeka punde tu Yeye alipofanya hivyo. Sauli wa Tarso, njiani mwake akiteremka, alibwagwa chini na hiyo Nuru kuu, kama nilivyosema jana usiku. Alijua huyo alikuwa ni Bwana. Akasema, "Bwana, U Nani Wewe?"

Kasema, "Mimi ni Yesu." Unaona?

261 Hiyo hapo Nguzo ile ile ya Moto, Nuru ile ile miongoni mwetu, akizaa Uzima ambao Hiyo ilizaa wakati Hiyo ilipokuwa ndani ya Kristo Yesu, ikifanya jambo lile lile katika Kanisa la Bibi-arusi leo hii. Unaona? Je! mtaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

262 Sasa naomba Bwana Mungu aje na anene kuhusu kile nilichonena juu Yake. Imani hiyo rahisi, sasa, Mungu Mbinguni anajua, unaona, kuamini tu hilo. Wakati Yeye alipokutana nami

huko juu, Yeye aliniambia hilo. Na mimi hapa nimesimama usiku wa leo, nimesimama, ninakisia hapa pana tatu—watu mia tatu, au zaidi, hapa ndani. Pia ni—ni—nimesimama mbele za nusu milioni, na kutoa changamoto hii, kote ulimwenguni. Na Yeye hataninii, Yeye haninii . . . Yeye ni Mungu. Hili, si kile ambacho nimesema, ni kile Yeye alichosema. Ni Neno Lake.

263 Sasa ninataka kila mtu awe tu na kicho, huku ninii . . . inapoendelea, kama inaendelea. Sasa, isipofanya hivyo, Yeye asipokuja, basi hakuna jambo moja niwezalo kufanya ila labda kuanzisha mstari wa maombi, kuweka mikono juu ya wagonjwa na kuwaombea, na kuenda nyumbani. Lakini hayo ndiyo yote niwezayo kufanya. Siwezi. Mimi ni mwanadamu. Mimi ni ndugu yenu. Mnaona?

264 Sasa, bali sasa ikiwa Roho Mtakatifu atafanya jambo fulani la kipekee, nanyi mnafikiri ni la ajabu, Mungu ni kitu cha kuabudiwa, mwabuduni Yeye kadiri mtakavyo.

265 Bali, sasa, na msipige picha zozote, msimulike nuru zozote, kwa sababu Hiyo ni Nuru. Ni wangapi wamewahi kuona picha ya Hiyo? Mnajua. Hakika. Iko Washington, DC. Unaona? Vema. Sasa kwa uchaji.

266 Na ningewatakeni nyinyi mlioko nyuma yangu mwombe kwelikweli sasa, maana ninaangalia wasikilizaji, na labda kesho usiku nitajaribu kuja huku, unaona.

267 Sasa, sijui. Mungu tu alifanya ahadi. Lakini ikiwa Yeye atajitambulisha Mwenyewe hapa, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu," na hiyo ndiyo njia pekee ambayo wewe . . . Huwezi kuiga huo, maana huo ni—huo ni mwujiza. Ni kitendawili. Kwa kweli ni kitendawili. Unaona? Kitendawili ni mwujiza, kitu ambacho hakiwezi kuelezeka.

268 Sasa hapa amesimama mwanamke. Sina fununu kidogo zaidi kile kilichomfanya mwanamke huyo kusimama hapo kuliko mtu yeyote mwingine aliyo nayo, isipokuwa kama ni mtu fulani hapa ambaye anamjua. Yeye ni mwanamke tu aliyesimama hapo. Lakini imetokea kuwa mwanamke. Inakuja niani mwangu, picha halisi ya Yohana Mtakatifu 4, mwanaume na mwanamke wakikutana, kama Bwana alivyokutana na yule mwanamke kisimani. Unaona? Sasa, kama mama huyu anayesimama hapa, na mimi si . . . Huenda akawa ni mgonjwa, labda yeye si mgonjwa. Labda ana shida ya kinyumbani. Labda ana shida ya kifedha. Ama labda amesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Si—si—sijui kilichomleta hapa. Siwezi kabisa kuwaambia, maana sijui. Sijui. Lakini yeye anajua.

269 Sasa kama nikija juu, kwa mfano, na kuweka mikono juu yake, na kusema, "Ninaweka mikono yangu juu yako, dada. Utukufu kwa Mungu! Huna budi kupona, kwa sababu Biblia ilisema, 'Weka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.' Amina. Nenda zako, ukishangilia. Umepona." Vema, anataka kuamini

hilo, hilo ni sawa, maana hilo ni Andiko. "Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Hiyo ni kweli. Hilo ndilo Biblia ililosema.

270 Lakini vipi ikiwa Roho Mtakatifu anasimama hapa na kumwambia jambo fulani ambalo amefanya, jambo fulani ambalo limekuwa huko nyuma katika maisha yake, kile ambacho amefanya, kile anachofanya sasa, kile kilichomleta hapa, kile anachotaka? Sasa, basi yeye anajua, atajua kama ni kweli au sivyo. Basi anajua hiyo haina budi kutokana na nguvu fulani za kimbinguni. Sasa inategemea kile anachotaka kuita hiyo, kama Beelzebuli; ama kama yule mwanamke kisimani, "Tunajua Masihi atafanya hili." Unaona, basi, chochote kile, hiyo ndiyo zawadi yake anayopata.

271 Lakini basi kama Yeye anaweza kumwambia kile ambacho amekuwa, na—na kama ni kweli, yeye atatambulisha kwamba ni kweli. Ndipo basi kama Yeye anajua kile ambacho huyo mwanamke amekuwa, hakika anaweza kumtumainia Yeye kwa kile Yeye asemacho kwamba mwanamke huyo atakuwa. Hiyo ni kweli? Kama mwanamke huyo anaweza kumtumainia Yeye kujua kile Yeye amekuwa, yeye anajua kama hiyo ni kweli au la, basi vipi kuhusu kile Yeye atakachokuwa?

272 Huu si ni wakati wa ajabu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unasema, "Kwa nini unasitasita, Ndugu Branham?" Ninamngojea Yeye. Hiyo ni hakika, hakika. Kama Hiyo isipokuja, siwezi kufanya hivyo. Hivyo tu, ninamngojea tu Yeye. Kweli. Unaona?

273 Hebu tuimbe ule wimbo wa kale wa kanisa, *Amini Tu*. Tupe sauti hapo.

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu.

274 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho hapa ndani chini ya udhibiti wangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa kaeni kimya kabisa.

275 Sasa, nyinyi mlioiona ile picha, (na nitakutana nanyi siku moja kwenye Kiti cha Hukumu cha Kristo), Huyo hayuko futi mbili kutoka mahali nimesimama sasa hivi. Hiyo ni kweli. Sasa kama huyo ni Roho Mtakatifu yule yule...Mtu yeyote anajua kwamba Malaika wa Agano alikuwa ni Yesu Kristo, Yule aliyeongoza Israeli kupitia nyikani. Basi ikiwa Yeye atakuja sasa. Na mimi nimedai kwamba Yeye ndiye ile Nuru. Sijui tu mahali Hiyo ilipo, lakini Hiyo ipo papa hapa karibu nami. Ninaihisi Hiyo, na ninajua ipo hapa.

276 Sasa kama Hiyo itachukua maisha yangu, mawazo yangu mwenyewe, utambuzi wangu, kila kitu kutoka kwangu, na kuzaa Yake Mwenyewe, basi Hiyo ni Kristo. Sasa je! nyinyi nyote

mtaamini, kama Yeye atafanya hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, sasa iweni na kicho kabisa. Itanibidi kuzungumza na mama huyu kwa kitambo.

277 Sasa yeyote yule aliye mhandisi wa maikrofoni hii hapa, iangalie. Kwa sababu, wakati ukiwa katika ono, wewe ni—wewe ni—wewe uko mbali na hapa. Uko mahali pengine, chini katika maisha ya mtu, mahali pengine, kama tu vile kuwa katika nchi nyingine, na inanibidi tu kuzungumza na kusema kile ninachoona. Ndipo basi kwa sababu itaniacha, na halafu sikumbuki kile ambacho nimesema, unaona. Kwa hiyo wewe angalia maikrofoni, yeyote aliye. Huku nikizungumza na mama huyu kama tu vile Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani, kuzungumza tu na yeye, kushika roho yake.

278 Kwa sababu, nilianza katika kuhubiri, muda mfupi uliopita, na hiyo kwa namna fulani. . .Kabla sijaondoka chumbani, siku moja, ninafunga na kuomba, na Hiyo iko karibu nami kabisa. Nami ninapaswa tu kuingia ndani moja kwa moja, nimwache mtu mwingine anene, na kisha niingie moja kwa moja mimbarani. Ni afadhali zaidi. Lakini kuwepo tu hapa usiku wa leo, halafu ni—ninataka kuzungumza na mama huyu.

279 Sasa, mama, Bwana Yesu ni mkuu. Na Yeye hajafa, bali Yeye yu hai milele. Unaamini hilo? Ni—ninaamini unaamini hilo. Sasa sisi tukisimama hapa, kama mwanaume na mwanamke ambao hawana budi kumkabili Kristo siku moja, ha—hatuna budi kumwona Yeye. Bali ninatambua kwamba wewe ni Mkristo. Kwa sababu, punde tu ninapoanza kuongea, basi ninahisi roho zao zikiingia ndani.

280 Sasa kama mama huyu atashuhudia kweli, hivi sasa anahisi hisia ya ajabu sana, kama tamu sana, yenye joto. Sasa kama mnaweza kutazama kwa macho yenu, nyinyi ambao hamjawahi kuiona Hiyo, Hii hapa moja kwa moja kati yangu na mama huyu, unaona, namna fulani ya Nuru ya kaharabu. Inatulia moja kwa moja juu ya mama huyu, sasa hivi. Pia, katika Jina la Bwana, anatambua kwamba kitu fulani kinamfanya ahisi utamu sana, tofauti na kile wewe. . .

281 Tu, unajua, uwepo wa ndugu yako usingeweza kufanya hilo. Kama hiyo ni kweli, inua tu mkono wako kwa watu. Unaona? Naam.

282 Sasa papa hapa, ninamwangalia mama huyu moja kwa moja, mawasiliano makamilifu na yeye. Mama huyo anafadhaika kuhusu jambo fulani, na hilo ni kwamba ametiwa uvuli. Kuna kivuli cheusi juu ya mwanamke huyo, na yeye anafadhaika. Naam, ni kansa. Ana kansa, nayo kansa hiyo iko kwenye mkono wake, kwenye kidole chake. Hiyo ni kweli, kwenye mkono wako. Huwezi kuiona hapa, lakini iko kwenye mkono wake, hata hivyo. Hiyo ni kweli.

283 Kwa nini, inabadilikabadilika, hata mtu fulani anafikiria . . . Usininii, usijaribu kuficha mawazo yako sasa. Ninaweza kuishika hapa kupitia Roho Mtakatifu. Mtu fulani alisema, "Alibahatisha hilo." Sikubahatisha hilo. Simjui mwanamke huyo. Sasa, sikubahatisha hilo. Sikubahatisha.

284 Vema, hapa, wewe ninii tu . . . Siwezi kuiona kutoka mahali nimesimama, iko kwenye . . .

285 Hapa, vema, weka mkono wako chini. Nitazame. Niamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu. Je! utafanya hivyo? Vema, hebu tuende mahali pengine. Naam, wewe ni mwaminio. Na unapaswa kuamini kwa ajili ya hiyo. Nilikuombea mara moja, muda mrefu uliopita, ukiwa na kansa, na ulipona.

286 Unasema, "Unamjua mwanamke huyo." Sikumjua. Sijawahi kumwona maishani mwangu, kadiri nijuavyo, ninamwona tu katika ono hili.

287 Hapa hebu nikuonyeshe jambo fulani. Anaye mtu fulani moyoni mwake, anayemwombea. Huyo ni mume wake. Yeye yupo hapa. Kama nitakuambia kilicho shida yake, je! utaamini kwamba ataponywa? Ana tatizo la tezi dume. Na hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Naam, Yesu Kristo akuponya.

288 Je! unaamini? "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! mnaamini Hiyo kuwa ni Mwana wa Mungu? Sasa ni wangapi wenu wanaoamini kwamba ni Yesu Kristo? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Iweni tu na imani. Msitie shaka. Mwaminini Mungu. Yeye ni mkuu tu leo hii kama Yeye alivyowahi kuwa.

289 Sasa wewe ulisema, kama tu vile, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yeye." Sasa, kama hiyo ilimfanya mwanamke kwenye kisima, chini ya hali ile, ha—ha—hali yake ya kiroho, kutambua hiyo kuwa ni ishara ya Masihi; na sisi wasomaji wa Biblia, na tumejazwa na Roho Mtakatifu, hiyo inapaswa kutufanyia nini?

290 Kama vile nimewazia mara kwa mara, wakati Mariamu akiwa na mimba kwa Roho Mtakatifu ambaye alimtia uvuli na kumwuumba mtoto huyu, akamwambia kuhusu kile kilichokuwa kinatendeka. Alikimbia juu kumwona binamu yake, Elisabeti, ambaye alikuwa miezi sita na—na Yohana, mke wa Zakaria. Nao walikuwa mabinamu. Na wakati Mariamu alipomwambia Elisabeti kwamba yeye pia alikuwa anaenda kumzaa mtoto, pasipo kumjua mwanaume, kwamba Roho Mtakatifu alikuwa anaenda kumleta, na kusema, "Waliita Jina Lake, 'Yesu.'" Mnajua, maskini Yohana, na yeye alikuwa miezi sita katika tumbo la uzazi la mama yake, na hakuwa amewahi kusogea bado. Unaona, hilo si kawaida; yapata miezi miwili au mitatu na mtoto anasogea. Lakini, hii ilikuwa si kawaida, maskini Yohana alikuwa mfu katika tumbo la uzazi la mama yake. Na punde tu salamu za Mariamu zilipokuja sikioni mwake, kasema, "Nitamwita Jina Lake, Yesu." Mara ya kwanza Yesu

Kristo lilipata kunenwa kwa midomo ya mwanadamu, ilimfufua maskini, mtoto aliyefariki, katika tumbo la uzazi la mama yake.

291 Hilo linapaswa kumfanyia nini mwanaume au mwanamke aliyezaliwa na Roho wa Mungu? Unaona? Hilo linapaswa kufanya nini wakati sisi tunajua tunaishi katika siku za mwisho, Maandiko yaliyolundikwa hapa kati—katikati yetu, usiku wa leo, juu ya sauti zetu hapa nje, kumwona Yesu Kristo akitupatia ishara ya mwisho kabla ya moto? Hilo linapaswa kutufanyia nini? Kutupeleka magotini mwetu, kwa toba.

292 Ninangojea tu kidogo, hakika, kwa namna fulani kujitikisa kutoka kwake, maana hunidhoofisha. Kama ilimdhoofisha Mwana wa Mungu, nguvu zilimtoka, ingenifanyia nini mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema?

293 Sasa huyu hapa msichana kama . . . Je! hii ndiyo inayofuata, hii ndiyo . . . U hali gani? Nilikuwa nimegeuka. Sikujua. Hatufahamiani mmoja na mwenzake, nadhani. Hatujuani. Sikujui. Na wewe ni mdogo kwangu kwa miaka, na labda tulizaliwa maili nyingi mbalimbali. Mara yetu ya kwanza kukutana. Lakini je! unaniamini kuwa ni nabii wa Mungu, ama, samahani, ninamaanisha mtumishi wa Mungu? Hilo huwakwaza watu, sababu . . . Hii iko kwenye kanda. Je! unaniamini kuwa ni mtumishi Wake?

294 Je! unaamini kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Na je! unaamini kwamba, wewe, Nuru hii ninayozungumzia, kwamba hiyo ndiyo Roho wa Mungu, Roho yeye yule, ile Nguzo ya Moto ambayo ilipitia nyikani pamoja na watoto wa Israeli, iliyodhihirishwa? Ile ile iliyokuja gerezani usiku ule, ile Nuru, pamoja na Simoni Petro, ikafungua milango ya gereza, ikamtoa nje, huru?

295 Je! unaamini siku moja Yeye ataingia na kutufanya huru? Ninaamini, pia. Aje kaburini na kufungua milango, nitatoka kutoka miongoni mwa wafu. Ninamtumainia Yeye. Yeye yupo hapa usiku wa leo. Si ni ajabu kujua kwamba haitubidi kuchukua filosofia fulani ya mwanadamu? Tunayo Biblia hapa inayonena hili. Na Yeye yupo hapa kutambulisha Kanisa Lake, kulipa imani ya kunyakuliwa ili kutwaliwa. Mtu anawezaje kukaa kimya!

296 Kuzungumza tu na mama huyo. Sasa, simjui. Huu hapa mkono wangu, sijawahi kumwona, kadiri nijuavyo. Ninii tu, kama sikujui na wewe hunijui, kusudi watu waseme . . .

297 Mtu fulani alisema, mwanaume yule niliyekuwa nikizungumza naye leo, huko chini akiokota mikebe, alisema, kwamba, "Watu walisema, 'Ndugu Branham huleta kundi lake mwenyewe pamoja naye, hivyo ndivyo yeye huwajua.'"

298 Kwa uchaji ninaapa mbele za Mungu, sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, kadiri nijuavyo, ama mtu yeyote mwingine katika mstari huo.

299 Kama hatufahamiani kabisa, dada, sikujui wewe wala chochote kukuhusu, inua mkono wako, kama sikujui nawe hunijui. Haya basi. Sijawahi kumwona mwanamke huyo. Vema.

300 Lakini ninamjua Mtu fulani aliyesimama hapa pamoja nasi, Ambaye anatujua sote wawili, Yeye ametulisha siku zote za maisha yetu. Ni Yeye ninayemtumainia. Ni Yeye ninayemwamini.

301 Sasa kama ningaliweza kukusaidia, na nisingefanya hivyo, nisingestahili kuzungumza kuhusu Neno hili. Mimi sistahili, hata hivyo. Lakini kama ningeweza kukusaidia, na nisingefanya hivyo, bali jambo la pekee ambalo ningeweza kufanya . . .

302 Kama Yeye alikuwa amesimama hapa, na wewe ulikuwa mgonjwa, ungesema, "Yesu, niponye." Yeye angesema, "Nimeifanya tayari wakati nilipokufa Kalvari." Yeye *ali*jeruhiwa kwa makosa yetu. Hapo gharama ililipwa, ilimalizika.

303 Lakini sasa Yeye angeweza kuthibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Yesu, kwa kukuonyesha ishara ya Masihi, kwamba Yeye alikuwa ni Yesu. Na Yeye aliahidi kufanya hivyo. Ni ninii . . . Jamani! Hakuna mwanya hata kwa ibilisi kuondoka, ndivyo? Yeye amefungiwa kwenye kona. Si Yeye ni wa ajabu? Ninataka . . .

304 Sababu nilikuwa nikisema hivyo, ninaona jambo fulani likitendeka. Mama huyo ndiyo kwanza aje kutoka kwenye upasuaji. Hiyo ni kweli. Je! hiyo ni kweli? Tatizo la kike, na wewe umefanyiwa upasuaji. Ume . . . Hiyo ni kweli? Pia unasumbuliwa na unyonge uliokithiri na wasiwasi. Hiyo si ni kweli? Ni vigumu kupona kutokana na hiyo. Nawe umekuja. Pia usiku wa leo, kabla ya kuja, uliomba uweze kufika hapa na kuombewa, katika mstari. Je! hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Sisomi mawazo yake. La, la. Kama nikikwambia kuwa wewe ni nani, kwa Roho wa Mungu, unajua kama ni kweli au si kweli, sivyo? Je! hiyo ingekufanya uamini? Hivi utaamini kwa moyo wako wote? Bibi Gideon, amini. Hiyo ni kweli. Nenda nyumbani, Yesu Kristo anakufanya mzima. Na uamini.

305 Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu tuseme, "Bwana asifiwe." ["Bwana asifiwe!"] Jamani, masalaale, nini . . . Kuwa tu na imani katika Mungu. Usitie shaka.

306 Kumbuka, hiyo ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Angalia kile Yeye asemacho. Unaona? Ono ni kitu kimoja, na BWANA ASEMA HIVI ni kingine.

307 U hali gani, bwana? Mimi ni mgeni kwako. Sisi ni wa jamii mbili tofauti, hata; kama mwanamke yule kwenye kisima, lakini Yesu alimfanya kujua. Mungu alifanya kwa damu moja watu wote. Mataifa na mahali tulipolelewa, na kubadilisha rangi zetu, hazina uhusiano wowote na sisi. Sisi ni ndugu, viumbe, vyote vilitoka kwa Adamu. Hiyo ni kweli. Bali jamii mbili tofauti

zinakutana hapa usiku wa leo, kama tu ilivyofanya wakati ule. Ikiwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anaweza kunifunulia kile ambacho umesimama hapo ukitaka, je! unaamini kwamba Yeye angekupatia? Unajua hilo. Asante, bwana. Unajua hilo. Vema, basi shida yako ya tumbo itakuacha, na kisukari chako kitatoweka. Rudi nyumbani.

"Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

308 Sasa mtu yeyote anaweza kuona, akisaidiwa hapa juu, kuna kitu ndani yake kinacholemaza. Sijui. Sijawahi kumwona mwanamke huyo. Yeye ni mgeni kabisa. Kama ningeweza kumponya, ningemponya. Siwezi. Sasa angalia huku, dada. Petro na Yohana. . .Hiyo tu ni kushika. . .Unaona, kuna watu kote, unaona. Ninamkumbuka Yeye akimwongoza mtu aliye kipofu nje ya mji, na kadhalika, unaona, amlete kwake Mwenyewe. Unaona, kila mtu ni roho aliye hai, unaona, na Hiyo inapaswa kukuchukua kutoka kwa imani kutoka kila mahali.

309 Sasa, mimi siwezi kuponya. Mnajua hilo. Mimi ni mwanaume, kama tu mume wa—wako angekuwa, baba yako, au yeyote mwingine. Mimi ni mwanaume, mwanadamu tu. Lakini Yeye ni Mungu. Hiyo ni kweli.

310 Sasa, ni kweli kwamba kulemaa kwako ni baridi yabisi. Na wewe—wewe una baridi yabisi. Ni mbaya, inazidi kuwa mbaya wakati wote. Hiyo ni kweli. Na jambo jingine, una hali mbaya kwelikweli ya wasiwasi. Una tatizo la kibofu. Hiyo ni kweli. Shinikizo kuu la damu. Unayo tu matatizo. Hiyo ni kweli. Hutoki hapa. La, umekuja kutoka California. Wewe rudi, na uamini. Unaenda kupona, katika Jina la Yesu Kristo. Kuwa na imani.

311 Unaamini? Vema, hebu tuinue tu mikono yetu na kusema, "Asante, Bwana Yesu." [Kusanyiko linashangilia—Mh.] "Pia, Bwana Yesu, tunakupa sifa na utukufu, kwa wema Wako wote na rehema kwetu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina." Kuwa tu na imani na usadiki.

312 Sasa mwangalie akiondoka akitembea. Angalia pale. [Kusanyiko linashangilia na kumsifu Bwana—Mh.] Unaona? Unaona? Semeni, "Bwana asifiwe." ["Bwana asifiwe!"] Amina.

313 Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye hasemi uwongo. Yeye husema kweli. Kile Yeye anachokuambia, kinaenda tu kuwa hivyo. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Kamwe hashindwi.

314 Sasa, mtu yeyote ambaye anaamini hilo, kama utalikubali, litafanya jambo lile lile kwako. Jambo pekee likupasalo kufanya ni kuamini. Sasa, kila mtu katika wasikilizaji anaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

315 Vipi kuhusu wewe uliye na mishipa iliyovimba? Unafikiri Mungu angeweza kukuponya kutokana na hiyo, akufanye mzima? Je! unaamini? Vema, itakuacha basi.

316 Ninataka kuwaulizeni, "Nani, alimgusa Nani?" Kamwe hakunigusa mimi. Hiyo ni kweli?

317 Vipi kukuhusu wewe, je unaamini? Unaamini maumivu hayo ubavuni mwako yatakuacha? Unasumbuliwa na maumivu ubavuni mwako. Vema, yatatoweka.

318 Ninakusai kuamini hilo, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, akijitambulisha Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Sikuwahi kumwona mwanamke huyo, sikuwahi kumwona mtu huyo. Waligusa nini? Walimgusa Kuhani Mkuu. Wako futi ishirini kutoka kwangu. Hawawezi kunigusa; hakungefaa kitu, hata hivyo. Bali walimgusa Kuhani Mkuu, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Yeye ni Yesu Kristo. Huna budi kuamini, hata hivyo.

319 Sasa mtu huyu, huyu hapa mwanaume, kama Simoni Petro. Labda mwanaume wa kwanza ambaye amekuja usiku wa leo, ninaamini. Mwanaume amekuja mbele hapa, kama Bwana Yesu; mwanaume, Simoni Petro alikuja mbele za Bwana Yesu. Mwanaume; nafikiri imekuwa ni wanawake, sasa ni mwanaume. Sasa kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, basi Yeye atakuwa tu kama Yeye alivyokuwa wakati ule. Hiyo ni kweli? Sasa simjui mtu huyu; Baba wa Mbinguni anajua hilo. Simjui. Yeye ni mwanaume tu aliyesimama hapa. Lakini Yesu Kristo anamjua. Basi ikiwa Yesu Kristo anaweza kunifunulia kile kilichomleta hapa, ama kitu fulani kumhusu, na—na Yeye atakinena, yeye anajua kama ni kweli au la. Mtu huyu atajua hicho. Na kama mtu yeyote hapa anamjua, watajua hicho. Bali mimi—mimi sijui hicho. Inanibidi tu kungojea. Lakini jibu lipo hapa. Lipo hapa, liko ndani ya Kristo. Hiyo ni kweli, nasi tunaliamini.

320 Na sasa hili ni jambo linalodhoofisha; linadhoofisha sana, sana. Nami ninatumaini ya kwamba utasadiki na kuwa na imani.

321 Sasa, bila kukujua, bwana. Na kama tu mtu alivyomleta Simoni juu mbele za Bwana Yesu. Sasa sisemi. . .Mimi siye Bwana Yesu, unaona. Mimi ni mwanadamu tu. Bali ninajaribu kusema kwamba Yeye yupo hapa miongoni mwa watu, nami ninawataka waone. Na ikiwa wanaweza kuona hilo, basi hakika wa—wanaweza kuamini na kukubali hilo. Wakati yote. . .Ikiwa ahadi hii, kama Yeye atafanya. . .Yeye hawezi tu akaja huko nje, na kutembea kuingia hapa ndani, aseme, "Ninaenda kukuponya *wewe*. Ninaenda kukuponya *wewe*." Ninii Yake. . . Hilo lingekuwa ni kinyume cha Neno Lake. Unaona, Yeye amefanya hilo tayari. Ananinii tu. . .

322 Kitu cha mwisho Yeye awezacho kufanya ni kuthibitisha tu kwamba Yeye yupo hapa kutimiza Neno Lake. Na ikiwa Yeye atatimiza hili na kulidhihirisha hapa mbele zenu watu wote, hakika mwanamke yule kiwete ambaye hata ilimbidi kuinua

kitu cha inchi nne pale, akiwa na baridi yabisi, akaruka juu chini na kukimbia kupitia hapa, kwa sababu ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Unaona? Yeye alimponya. Sasa hakika unaweza kuamini kwamba Yeye yupo hapa.

323 Sasa mwanaume huyu, mgeni kwangu, na mimi kwake. Sote wawili hatufahamiani. Sasa ikiwa Bwana Yesu atafunua hilo, acha yeye awe mwamuzi. Basi je! nyinyi nyote mtaamini na kukubali uponyaji wenu, chochote kile, mtaamini kwa ninii yote . . .

324 [Ndugu Branham anatulia—Mh.] Mama fulani alionekana hapa mbele zangu. [Ndugu Branham anatulia.] Mama huyo hapo aliye na shida ya pafu, amini kwa moyo wako wote na Yesu Kristo atakufanya mzima, kama unaweza kuamini. Unaamini hilo? Mimi ni mgeni kwako, lakini Yesu Kristo anajua kile ulichokuwa ukiwazia. Sasa wewe amini, na utakuwa mzima. Amina. Amina.

325 Si Yeye ni wa ajabu? Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye ni mama tu aliyeketi hapo. Lakini yeye . . .

326 Hebu niwaambieni jambo. Mwanamke huyo alikuwa ameketi hapo, akisema, "Bwana, jalia nikuguse Wewe." Mwulize kama hiyo si kweli. Jambo ndilo hilo. Hiyo ni kweli.

327 Ndipo nikamwona akitokea hapa, na kusikia kile alichosema. Na kuangalia nyuma, na nikawazia, "Yuko wapi mtu anayeonekana namna hiyo?" Nisingeweza kuiona popote. Na nikaendelea kuangalia. Na wakati yeye angeweza . . . Niliangalia kote, na moja kwa moja niliiona ile Nuru ikisonga huko na kuning'inia juu ya mwanamke huyo. Alikuwa huyu hapa, unaona. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina. Bwana Yesu anajua kila kitu.

328 [Mtu fulani anasema, "Mama huyo alikuja pamoja na mimi."—Mh.] Hilo ndilo lililokuwa. Mwanaume huyu anasema mama huyo alikuja pamoja na yeye. Amina. Hilo si ni jambo fulani? Unaona? Sasa si . . . Si hiyo ni ajabu? Bwana Yesu anajua mambo yote. Hivi hamwoni? Huyo hawezi kuwa ni mimi, marafiki. Mnajua hilo. Wewe—wewe ni mwerevu kuliko hapo. Unajua hilo.

329 Sasa kwa mwanaume huyu anayesimama hapa. Sasa, nikiwa sikujui, na bila kujua chochote kukuhusu, kama Bwana Yesu atanifunulia kitu fulani kilichokuleta hapo, au kitu fulani ambacho umefanya kusababisha tatizo lako, ama chochote kile, basi unajua kwamba Yeye, inabidi iwe ni Bwana Yesu. Hiyo ni kweli. Vema, sasa naomba Yeye ajalie hilo.

330 Kitu cha kwanza, mwanaume huyo anasumbuliwa na u—ugonjwa wa damu. La, ni shinikizo la damu. Anaugua shinikizo la damu. Pia ana jambo fulani kasoro na mwili wake. Ninamwona ameketi huku ameinua miguu yake, ama

baadhi. . .Loo, ni—ni maji yanajikusanya karibu na vifundo vyako vya mguu, kote namna hiyo. Naona, wewe ni mhudumu, mhubiri wa Injili. [Ndugu huyo anasema, "Amina."—Mh.] Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? Kasisi Williams, kama unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuondoka kutoka hapa na uwe mzima. [Kusanyiko linashangilia.] Mungu akubariki. Amina.

Je! mnaamini? [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

331 Je! unaamini kwamba Mungu huponya kansa? Je! unaamini Yeye huponya kansa na kuwafanya watu wazima? Nenda ukitoka jukwaani, ukiamini, na uponywe. Amina. Amini kwa moyo wako wote.

332 Je! unaamini Mungu huponya ugonjwa wa moyo? Unaamini? Vema, basi wako umeponywa. Nenda na uamini kwa moyo wako wote. Sifa tu iwe kwa Mungu! Amina.

333 Sasa, ulikuwa na hisia ya kigeni kwelikweli wakati nilipomwambia mtu huyo hivyo, kwa sababu ulikuwa na ugonjwa wa moyo, pia. Kama utaendelea kuamini, hautarudi. Utakuacha kabisa. Nenda, amini kwa moyo wako wote. Amina. Vema.

334 Mwanamke huyu anayekuja hapa ametiwa uvuli wa mauti. Alikuwa na kansa, lakini sasa imetoweka. Amini kwa moyo wako wote, nayo itaondoka, na uwe mzima. Kama hutatilia shaka, haitarudi kama hutatilia shaka, bali uamini.

Njoo, mama.

335 Sasa unasema nilikuwa "ninasoma mawazo ya watu." Igeuze hivi. Yule Malaika wa Bwana aliyepaswa kuja katika siku za mwisho, Bwana Mungu Yehova, alipaswa kujua kilichokuwa nyuma Yake, kama Yeye alivyofanya. Mwanamke huyu yuko nyuma yangu.

336 Amini, dada. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Kama unaamini, inua mkono wako?

337 Mama huyu nyuma yangu, je! ameinua mkono wake? [Mtu fulani anasema, "Naam."—Mh.] Kama Bwana anaweza kunifunulia, nikiangalia upande *huu*, shida ya mwanamke huyo, mtaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Ndiyo."] Analo tatizo la kike, shida ya kina mama.

338 Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako, mama huyu hapa. Umepona sasa, na Yesu Kristo anakufanya mzima. Utukufu kwa Mungu! "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu."

339 Mahali hapa usoni mwake pamegeuka kuwa kansa. Kama angeamini kwa moyo wako wote, unaweza kuenda, nayo itakuacha, nawe utakuwa mzima. Siwezi kuponya, lakini Mungu atakuponya kama utaamini kwa moyo wako wote. Mimi si mponyaji. A-ha. Amina.

340 Je! mnaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

341 Dada, angalia huku, mama. Unaugua baridi yabisi, ni mbaya sana asubuhi, wakati unapojaribu kutoka kitandani. Unachomeka mguu mmoja, na halafu unajaribu kufanya njia yako, na kushikilia vitu wakati mwingine, ndani ya nyumba, ukijaribu kutembea. Hiyo ni kweli kabisa. Kama utaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakufanya mzima. Kesho alasiri itakuwa tofauti, kama utaamini hilo.

342 Hebu tuseme, "Bwana asifiwe." [Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe," na kushangilia—Mh.]

343 Mwanaume huyu ana umri mkubwa. Ana ugonjwa uitwao tezi dume, ambao ni umri kwa uume wake. Anayo mambo mengi kasoro kwake. Bali mojawapo ya mambo makuu ambalo ananitaka nimwombee kwa ajili yake, ni baridi yabisi. Imekuwa ikimsumbua kwa muda. Hiyo ni kweli. Je! unaamini? Nenda zako na uponywe. Na umshukuru Yesu Kristo, huwafanya wagonjwa kuwa wazima! . . . ? . . . Vema, bwana.

344 Simjui maskini msichana huyu, mtoto anayeonekana mwenye afya. Nitazame na uamini, mama. Je! unaamini kwa moyo wako wote? Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida Yako? Uko karibu kurukwa na akili, kutokana na hali ya wasiwasi. Ibilisi amekudanganya, anajaribu kukufanya ufikirie kuwa unarukwa na akili, na kila kitu. Usiamini hayo. Uko huru. Yesu Kristo anakufanya huru. Amina.

345 Je! mnaamini, wasikilizaji wote? Mnaamini sasa, katika Uwepo Wake? [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

346 Je! unaamini kwa moyo wako wote, dada? Je! unamwamini Yeye? Unaamini? Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe. Amina. Amini kwa moyo wako wote.

347 Ana wasiwasi, analo tatizo la kike, pia anaugua baridi yabisi. Iko karibu kumlemaza. Kama ukiamini kwa moyo wako wote, unaweza kwenda uwekwe huru. Je! unaamini hilo? Basi, nenda katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Ninaamini amenyooka, na kupona.

348 Je! mnaamini kwa mioyo yenu yote? Sasa ngojeni. Je! Yesu Kristo hutimiza Neno Lake? Hivi Yeye hutimiza Neno Lake? Ni wangapi wanaamini kwamba ni Yeye yule? Ni wangapi wanaamini kwamba mnamwona Yesu Kristo akifanya kazi miongoni mwa watu Wake? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

349 Sasa, ninawaambieni kweli. Hakika tu unaweza kuamini kama Mungu akikuambia kuwa ninasema kweli. (Sasa ninamhisi mwanangu ama mtu fulani akivuta kwenye koti langu, ambalo linamaanisha kwamba ni wakati wake kuniacha

niende.) Ninataka kuwaambia kweli, hilo ni Neno la Mungu lililoahidi kufanya hivyo.

350 Neno pia liliahidi hili. Mliinua mikono yenu na kusema mlikuwa ni waaminio. Je! hiyo ni kweli? Maneno ya mwisho Yesu aliyosema, kabla hajapaa Juu, Yeye alisema aliwapa wanadamu vipawa, Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Je! hiyo ni kweli? "Kama wao," waaminio.

351 Ni wangapi ambao ni waaminio, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi wewe weka mkono wako juu ya mtu fulani karibu na wewe. Weka tu mkono wako juu ya yule aliye kando yako. Wekeaneni mkono mmoja juu ya mwenzake. Loo, sasa mwombee mtu huyo.

Bwana Yesu, jalia hilo, Bwana.

352 Shetani, toka ndani ya kundi hili la watu, katika Jina la Yesu Kristo.

[Kusanyiko linaendelea kuomba na kushangilia—Mh.]

Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele SWA63-0627
(Jesus Christ The Same Yesterday, Today, And Forever)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 27 Juni, 1963, kwenye Uwanja wa Mikutano wa Associated Brotherhood Of Christians kule Hot Springs, Arkansasa, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org